# Nipashe

Jumanne Januari 21, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581928

www.ippmedia.com 0677 020 710 MWANGA WA JAMII

Nipashe digital LIKE & FOLLOW US

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ




**MBAPPE RASMI AKIRI KUIZOEA REAL MADRID**

UKURASA 21

RIPOTI MAALUMU - 2

**Kilichojificha** taka hatari za hospitalini kutapakaa ufukweni

UKURASA 4

**Askofu** Malasusa afunguka kiini cha baa la ndoa nyingi kuvunjika

UKURASA 5

UGENI MIKOA SITA

**Msaada** kisheria wa Mama Samia kuanza wiki hii

UKURASA 8

epaper.ippmedia.com MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com

# Hukumu ya CHADEMA

• **Timu** Mbowe, Lissu zatambiana kumaliza ubishi leo; Odero anyatia kiti kimyakimya... *ukurasa 3*



Freeman Mbowe




Charles Odero



Tundu Lissu

## Mshukiwa video ya utupu wanafunzi Baobab mbaroni

UK. 8



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na waandishi wa habari baada ya mazungumzo yake na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Dk. Tedros Ghebreyesus (kushoto), Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. **Habari Uk. 2. PICHA: IKULU**

# Samia atoa angalizo CCM

UK. 2

**MICHEZO** **YANGA: AHSANTENI, HAIKUWA RIZIKI CAF** UK.24

**MAONI,** UK.6

# Samia atoa angalizo CCM

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Samia Suluhu Hassan ameelekeza masuala manne ya kutafakari na kufanyia kazi kwa viongozi wa chama hicho, ikiwamo kuzingatia miiko, kupinga dhuluma na uonevu wakati wa Uchaguzi Mkuu.

Mambo mengine ni tahadhari dhidi ya matumizi mabaya ya Akili Mnemba (AI) wakati wa uchaguzi, kuwaeleza wananchi namna serikali ilivyotekeleza ilani na kudumisha umoja.

Akifunga Mkutano Mkuu Maalumu wa siku mbili juzi jijini hapa, Rais Samia alisema viongozi wa CCM lazima waoneshe matendo mema na kuwa mfano bora wa kuigwa katika jamii kwa kupinga waziwazi dhuluma na uonevu na hujuma dhidi ya mambo mazuri yaliyomo nchini, ili kuwa na kauli thabiti kwa wanaotenda maovu.

"Kama sisi viongozi hapa, wewe ni mjumbe wa Mkutano Mkuu umetoka huko ulikotoka, wewe siyo mtu mdogo, hiki ndicho kikao cha juu kabisa cha chama chetu. Mkisema Kamati Kuu na Halmashauri Kuu laleni kwenye makapeti tutalala kwa sababu ninyi ni waajiri wetu

"Ukiwa mjumbe wa Mkutano Mkuu, cheo chako ni kikubwa sana, niwaombe sana tuendane na hadhi ya chama chetu, sisi sote wakati tunaomba kuwa wanaCCM tulitoa ahadi kwa chama hiki, zipo kwenye Katiba na kadi zetu, sifa na miiko ya kiongozi hasa tunapoelekea kwenye Uchaguzi Mkuu," alisema.

Aliongeza kuwa nchi ina uhuru mpana wa vyombo vya habari, hivyo wanapovitumia wawe makini wasitoe kauli zitakazosababisha utata kwa jamii na tafsiri isiyokusudiwa.

"Unaweza kusema jambo, sentensi yako ikawa na maudhui mchanganyiko, mwandishi asiye na nia njema akaamua kukata kipande kidogo cha yale uliyoyasema akayasambaza akakuharibia na kukitia doa chama chetu, niwaombe sana ndugu zangu umakini katika chama chetu," alisema.

Vilevile, alisema ukuaji wa teknolojia hasa Akili Mnemba, umekuja na mambo



mengi, ikiwamo kuigiza sauti ya mtu na hata kusema mambo ambayo hajayasema.

"Tumeshuhudia kampeni kwenye nchi kubwa moja kule, tuliona mgombea mmoja anasemeshwa maneno kwamba anasema nikimshinda huyu atakwenda kuishi Zanzibar, Mama Samia mpokee huko mweke huko, huko Mama Samia wala hajulikani kihivyo, lakini ni matumizi ya Akili Mnemba," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema kuwa mwaka huu wa uchaguzi anaamini matumizi ya teknolojia hiyo yatakuwapo na yanaweza kutumika vibaya kueneza uzushi na uchochezi.

"Pamoja na vyombo husika vikiendelea kuweka mikakati ya kushughulikia masuala haya ni vizuri, sisi wana CCM kujua hatari hiyo ili itakapotokea isitutoe kwenye mstari," alisema.

Mwenyekiti huyo pia aliwataka kudumisha umoja ndani ya chama na kwamba katika mchakato wa uchaguzi watakapopatikana wagombea, wawe wamoja ili kutafuta dola na kushinda.

Kuhusu utekelezaji ilani, Mwenyekiti Samia alisema wajumbe wa mkutano huo wana wajibu wa kueleza namna serikali ilivyotekeleza ilani ya uchaguzi kwa wananchi wa maeneo yao.

Pamoja na hayo, Mwenyekiti Samia aliwashukuru wajumbe kwa imani waliyoonesha kwake na Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Mwinyi na kwamba miaka mitano ijayo watakapochaguliwa watafanya zaidi.

"Lengo ni kuhudumia wananchi wetu na kuinyanyua nchi yetu kiuchumi, kisiasa na kijamii," alisema.

Akizungumzia kupumzika kwa Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, Rais Samia alimshukuru kwa kazi kubwa aliyofanya ya kumsaidia kwenye sekta za kiuchumi kwa kuwa ni mchumi bobezi.

"Na alivyoomba kupumzika wakati ukifika tumwombe Mungu yale matamanio yake moyoni mwake yakatimie, apumzike vyema! Mungu ampe umri mrefu, afya njema na furaha ya moyo wake, tunakushukuru sana kwa utendaji kazi wako ndani ya taifa lako," alisema.

Aliwataja marais wastaafu (Jakaya Kikwete, Amani Abeid Karume na Dk. Ali Mohamed Shein) wamemsaidia kwenye mkutano huo kutokana na alivyoshtuka baada ya wajumbe kuja na hoja ya kutoa azimio la kuwapitisha kuwa wagombea wa urais yeye na Dk. Mwinyi kwenye Uchaguzi Mkuu mwaka huu.

"Nilipowaita chemba pia wamenisaidia sana, hapa niwashukuru sana na pengine nimshukuru Kikwete kwa sababu wazo hili lilikuja wakati yeye akiwa mwenyekiti wa chama, aliunda kamati ya wazee wa chama ambapo viongozi waliokuwapo wakikwama wanakimbilia kwao, wao ni 'encropedia' ya chama hiki, ukienda kwao hukosi ufumbuzi," alisema.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***

## Rais aihakikishia WHO Tanzania iko salama

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan amewahakikishia watanzania na jumuiya za kimataifa kuwa Tanzania ni eneo salama licha ya kubainika kisa kimoja cha mtu aliyeambukizwa virusi vya ugonjwa wa Marburg wilayani Biharamuro, mkoani Kagera.

Amesema hatua zilizochukuliwa mwaka 2023 kudhibiti virusi hivyo wakati vilipobainika nchini, zimeiwezesha Tanzania kuwa na uzoefu wa kutosha kudhibiti maambukizi.

Rais Samia aliyasema hayo jana Ikulu ya Chamwino, wakati akizungumza na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Dk. Tedros Ghebreyesus.

"Serikali ilituma timu ya wataalamu Januari 11 mwaka huu, kuchunguza kuhusu ugonjwa huo ambapo katika sampuli zilizochukuliwa, mgonjwa mmoja pekee ndiye aliyekutwa ameambukizwa," alisema.

Rais alisema hatua kadhaa zimechukuliwa ikiwamo kufanya uchunguzi kwa kufanya kazi karibu na mamlaka za serikali za mitaa, kuanzisha kikosi kazi cha dharura, kupeleka timu ya uchunguzi kufanya tathmini ya hali halisi kisha kutoa taarifa kwa umma.

Dk. Ghebreyesus alisema kuwa kutokana na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Tanzania katika kudhibiti maambukizi hayo, WHO imetoa dola za Marekani milioni tatu kuongeza nguvu katika mapambano hayo.

Alisema Tanzania ina uzoefu wa kutosha kukabiliana na maambukizi hayo na ndiyo sababu WHO inaunga mkono juhudi za serikali.

Dk. Ghebreyesus pia alimpongeza Rais Samia kwa kuendelea kuboresha huduma za afya kwa kupitisha Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ambayo itatoa hakikisho kwa wananchi kupata huduma za afya kwa uhakika.

# ...Uteuzi CCM wawaibua wadau

**Na Waandishi Wetu**

WADAU wa siasa wamesema uamuzi wa kupata wagombea urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mapema ni turufu kwa chama, huku wakisifu uteuzi wa Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi kuwa mgombea mwenza.

Mchambuzi wa masuala ya siasa na uchumi nchini, Dk. Albanie Marcossy, alisema uamuzi wa kuwapata wagombea kwa kushtukiza na mapema ni ishara uchaguzi ujao hautakuwa mwepesi.

Askofu wa Kanisa la Baptist Tanzania Kanda ya Kati, Antony Mlyashimba, alisema Mkutano Mkuu Maalumu wa CCM umefanya jambo jema kwa mujibu wa kanuni za chama hicho, majina ya wagombea yamefahamika mapema. Itawasaidia wanachi kuwafahamu vizuri ili kuwachagua kwenye Uchaguzi Mkuu.

"Jambo lililofanywa na chama hiki ni zuri, kama inawezekana ipo haja ya kubadilishwa kwa sheria, ili michakato hii ianze mapema kwa vyama vyote kutambulisha wagombea wao ili wafahamike na wapigakura wao. Mgombea wa nafasi ya urais si vizuri kuwa wa kushtukiza, lazima tumjue mapema.

"Maana hata wenyewe CCM jana (juzi) kwenye mkutano wa kupitisha majina hayo kulikuwa na sintofahamu, hivyo ipo haja kama kuna uwezekano kufanyike marekebisho, ili kusiwe na ukakasi kama uliotokea jana maana hata Rais mstaafu Jakaya Kikwete hakuwa na majibu ya moja kwa moja," alisema.

Hassani Mbangile, mkazi wa Manispaa ya Mtwara Mikindani, alisema demokrasia ndani ya CCM inapaswa kuzingatia taratibu za ndani za chama hicho.

Alisema chama hicho kilipaswa kutoa nafasi kwa wagombea wengine kugombea nafasi ya urais badala ya kupitisha jina moja la mgombea wa urais, jambo ambalo anaona ni kuminya haki za wanachama wengine ambao wanataka majukumu hayo.

Mkuu wa Kitivo cha Ushirika na Maendeleo ya Jamii ya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Dk. Cyril Komba, akizungumzia uteuzi huo na sura yake kisiasa nchini alisema:

"Hii inaonesha jinsi gani CCM iko makini. Kwa uteuzi wa Balozi Dk. Nchimbi, Rais Samia Suluhu Hassan au CCM imefanya jambo la maana sana. Nchimbi amekulia kwenye chama tangu akiwa kijana.

"Hakuna asiyefahamu umahiri wake katika kukisaidia chama kishinde uchaguzi, amekuwa ni nguzo kuu katika ushindi wa CCM tangu akiwa kijana Umoja wa Vijana (UVCCM), akawa waziri, balozi na sasa Katibu Mkuu wa Chama. Kwa hiyo nafikiri chama kimelamba dume."

Mkazi wa jijini Dodoma, Bashiru Kajuna, pia alipongeza mkutano mkuu kwa kupitisha jina Balozi Nchimbi, kuwa mgombea mwenza kwenye Uchaguzi Mkuu 2025.

Mwanazuoni na mchambuzi wa masuala ya kisiasa kutoka jijini Mwanza, Pius Lufutu alisema hatua hiyo ya juzi ya CCM ni mkakati katika kuufikia mchakato wa uchaguzi.

Alisema kuwa kwa mujibu wa chama hicho, mabadiliko yoyote ya kikatiba yanaweza kufanyika muda wowote kutokana na makubaliano ya kamati kuu za chama hicho.

"Tunaweza kujiuliza kwanini wamefanya mapema hivi badala ya utaratibu wa kawaidi wa mwezi Mei, majibu ni kuwa kwa upande wa CCM wenyewe wamefuata matakwa ya kikatiba kuwashirikisha wajumbe wote wa kamati tendaji ya chama hicho ambao wameridhia mabadiliko madogo kwa manufaa ya chama," alisema.

***Imeandikwa na Godfrey Mushi (ARUSHA), Paul Mabeja (DODOMA), Vitus Audax (MWANZA) na Baraka Jamali (MTWARA).**

HABARI KITAIFA

# Siku ya hukumu CHADEMA leo

**Na Elizabeth Zaya**

NI siku ya hukumu! Baada ya tambo za muda mrefu, leo sanduku la kura linaamua nani awe Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Freeman Mbowe ameomba achaguliwe tena kukiongoza chama hicho, akikabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa wanasheria Tundu Lissu na Odero Charles. Wajumbe wa Mkutano Mkuu 1,328 ndiyo wamebeba si tu nafasi za watatu kisiasa, bali pia kinachotajwa hatima ya CHADEMA.

Kati ya wajumbe hao, ni 792 ni kutoka majimbo la uchaguzi, 124 wilaya za kichama, 68 mikoa ya kichama, 30 kanda za kichama, 99 wa mabaraza na 15 wa Kamati Kuu. Wote watawachagua Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti Bara na Zanzibar.

**TIMU MBOWE, LISSU**

Baadhi ya sababu zinazotolewa na wanaomuunga mkono Mbowe wanasema ni mbunifu, ndiyo sababu chama hicho kinaendelea kuwa imara kwa miaka mingi.

Baadhi ya hoja ambazo zimekuwa zikitolewa na wafuasi wanaomuunga mkono Lissu ni pamoja na mvuto alionao kutokana na sera zake zinazolenga mabadiliko ya kweli ndani ya chama na taifa lake.

Lissu, pamoja na mambo mengine, ameahidi kushusha fedha za ruzuku ya chama hadi ngazi ya majimbo, ukomo wa madaraka hasa kwenye nafasi za ubunge wa viti maalumu na ujasiri wa kupambana na vitendo vya rushwa ndani na nje ya chama chake.

**SERA ZA ODERO**

Mbali na Mbowe na Lissu, mgombea mwingine wa nafasi hiyo ya uenyekiti ni Odero. Ahadi zake ni pamoja na kuwawezesha watanzania kupata mahitaji manne muhimu ikiwamo uwezo wa kupata chakula bora, mavazi, makazi na uwezo wa kuwasiliana.

Nyingine ni kusimamia madhumuni ya chama chake, kushika dola, kupigania watanzania kwa kupinga tozo za miamala ya simu zisizoainishwa na serikali.

**BARAZA KUU**

Katika nyakati za lala salama jana, akifungua mkutano wa Baraza Kuu uliofanyika Dar es Salaam, Mbowe aliendelea kusisitiza kuwa hakuna mkubwa kuliko chama hicho huku akiwatahadharisha wanachama wasitoe nafasi kwa yeyote mwenye nia ya kukipasua chama hicho.

"Tusitoe nafasi kwa yeyote mwenye dhamira ya kukipasua chama, tumesema na ninarudia chama hiki kina thamani kuliko yeyote miongoni mwetu, kwani kimebeba ndoto za watanzania.

"Kwa hiyo ndugu zangu wana-CHADEMA, tumekuja Dar es Salaam si kupaniana, tumekuja kuyajenga, kwamba chama hiki tutakipigania, tutakijenga, tutakipanga, tunapotofautiana tutazungumza, ili mwisho wa siku kikabebe ndoto ya taifa letu ya haki, demokrasia kwa kila mmoja na hatimaye maendeleo ya watu wetu wote," alisema.

> **Lissu, pamoja na mambo mengine, ameahidi kushusha fedha za ruzuku ya chama hadi ngazi ya majimbo, ukomo wa madaraka hasa kwenye nafasi za ubunge wa viti maalumu na ujasiri wa kupambana na vitendo vya rushwa ndani na nje ya chama chake.**

**WALIOKATWA WALALAMA**

Baadhi ya wagombea ambao hawakuteuliwa katika nafasi ya ujumbe wa Kamati Kuu, wamelalamika hawajatendwa haki huku wakiomba uchaguzi usimame mpaka majina yao yarejeshwe.

Wagombea waliokatwa ni pamoja na Mwangasa, Twaha Mwaipaya, Dk. Msofe, Rose Mayemba, Adamu Chagulani na Hossiana Kusiga.

Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika alitolea ufafanuzi jambo hilo, akisema: "Ninaomba kuhakikishia kuwa usaili na uteuzi uliofanywa na Kamati Kuu, Januari 19 mwaka 2025, ulifuata utaratibu uliopo katika katiba na kanuni za chama na kutumia demokrasia kama nyenzo ya uamuzi katika siasa."

Mkutano huo wa Baraza Kuu baada ya kufanya usaili, uliwateua Mbowe, Lissu na Odero kugombea nafasi ya Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa huku walioteuliwa katika nafasi ya Makamu Mwenyekiti Bara ni Ezekiah Wenje, John Heche na Mathayo Gekul na kwa nafasi ya Makamu Mwenyekiti Zanzibar walioteuliwa ni Hafidh Ali Saleh, Said Issa Mohammed, Said Mzee Said na Suleiman Makame Issa.

Jana, wenyeviti 17 wa mikoa walitangaza kumuunga mkono Mbowe, huku juzi wenyeviti 21 walitangazwa na mwanachama wa CHADEMA, Godbless Lema kuwa wanamuunga mkono Lissu.

*Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*


AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
benki kwa maendeleo yako

## TAARIFA KWA UMMA

### Kuunganishwa Matawi yaliyoko Kariakoo and Ubungo jijini Dar es Salaam

Akiba Commercial Bank Plc inapenda kuwajulisha wateja wake na umma kwa ujumla kuwa Benki itaunganisha matawi yafuatayo yaliyopo jijini Dar es Salaam ifikapo tarehe 22 Februari 2025:

- Matawi ya Ilala na Aggrey yataunganishwa na Tawi la Kariakoo, lililopo pembeni ya Jengo la China Plaza, Barabara ya Uhuru.
- Tawi la Tandale litaunganishwa na Tawi la Ubungo, lililopo Ubungo Plaza, Barabara ya Morogoro.

Uamuzi huu ni sehemu ya juhudi zetu za kimkakati za kuboresha huduma, kuongeza ufanisi na kukuza matumizi ya huduma za kidigitali. Katika mabadiliko haya, akaunti za wateja wa matawi ya Ilala na Aggrey zitahamishiwa tawi la Kariakoo na akaunti za wateja wa tawi la Tandale zitahamishiwa tawi la Ubungo.

Benki inapenda kuwahakikishia wateja wake na wadau wote kuwa zoezi hili halitaathiri huduma za kibenki au matumizi ya akaunti na Benki itatoa msaada mahsusi kadiri utakavyohitajika wakati wote wa zoezi hili. Benki inawahimiza wateja kuendelea kutumia huduma zetu za kidigitali kama vile ACB Mobile, ACB Internet Banking ACB VISA Cards na Akiba Wakala.

Tunawashukuru wateja wetu kwa kuendelea kutuamini. Tunaendelea kuwaahidi utoaji wa bidhaa na huduma bora ili kutimiza mahitaji yenu ya kifedha.

Kwa maelezo zaidi, tembelea tovuti yetu www.acbbank.co.tz, kurasa zetu za mitandao ya kijamii, au wasiliana na Meneja wa Tawi, Afisa Uhusiano, au Kituo chetu cha Huduma kwa Wateja kupitia nambari yetu ya bila malipo (Toll-Free Number) 0800 750 336.

**Dora Saria**
**Mkuu wa Masoko na Mawasiliano**
**Akiba Commercial Bank Plc**

218333302

RIPOTI MAALUMU - 2

# Nyuma ya pazia kutapakaa ufukweni taka za hospitalini

Na Jenifer Gilla

**SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii jana iliangazia madhara ya taka hatarishi za hospitalini zinazotapakaa kwenye ufukwe wa Rainbow, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam. Endelea kupata undani wa uchafuzi huu wa mazingira...**

---

BAADHI ya vituo vya kutolea huduma za afya vinatupa taka hatarishi za hospitalini kwenye mito na vijito na kuwa chanzo cha uchafuzi wa fukwe za Bahari ya Hindi mkoani Dar es Salaam.

Huku kukiwa na sheria zinazoelekeza taratibu maalumu za kuhifadhi, kukusanya, kurejeleza na kuteketeza taka hizo, mikono ya wanaopaswa kuchukua hatua inaonekana kufa ganzi.

Katika ufuatiliaji wake ndani ya Manispaa ya Kinondoni, mwandishi wa habari hii amebaini taka hizo zikishamwagwa katika vijito, husombwa na maji hadi kwenye mito; Mbezi, Feza, Mpiji na Mlalakua inayomwaga maji katika Bahari ya Hindi.

Taka hizo zikishamwagwa baharini na mito hiyo, hukita kwenye fukwe, ukiwamo wa ufukwe wa Rainbow. Bahari haihifadhi uchafu.

Ramadhani Juma mwenye makazi jirani na ufukwe huo, anasema taka hizo hupelekwa baharini na katika mito, hasa mvua kubwa inaponyesha.

Anadai chanzo cha taka hizo ni baadhi ya wamiliki wa vituo vidogo vya kutolea huduma za afya katika manispaa hiyo na maeneo jirani ambao hawafuati utaratibu wa kudhibiti taka hizo, akidai huwalipa fedha kidogo wazoa taka wa mitaani wakazitupe.

"Unakuta mwenye zahanati, kituo cha afya au hospitali anaona kuliko atoe Sh. 50,000 kwa ajili ya kupeleka taka zake sehemu husika, anampa mwendesha mkokoteni Sh. 5000 bila kujali atakwenda kuzitupa wapi. Matokeo yake wanakwenda kuzimwaga kwenye mifereji na mito ambayo huzileta huku kwenye fukwe," Juma anasema.

Maimuna Ally anayefanya biashara ya chakula katika ufukwe wa Rainbow, anashauri serikali iangalie uwezekano wa kudhibiti wanaotupa taka katika Mto Mbezi anaoutaja kuwa ndiyo sababu ya taka nyingi zinazoonekana katika ufukwe huo.

Hawa Abdalah, mwuzaji wa chakula katika ufukwe wa Rainbow, anasema taka hatarishi kwenye ufukwe huo huwa nyingi zaidi mvua kubwa ikinyesha.

"Mabomba ya sindano yanayozagaa katika eneo hili ni hatari kwa sababu mtu akichomwa na hizi sindano, anaweza kupata maambukizi ya magonjwa hatari," Hawa anaeleza uzoefu wake.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mbezi Beach A, Mohamed Mzee anasema uchafu huo unatoka kwenye mito, ukiwamo Mto Mbezi.

Hata hivyo, mwenyekiti huyo anasema wanaendelea kuchunguza kubaini anayetupa taka hizo hatarishi za hospitalini ili wachukue hatua za kisheria.

Mzee anashauri Wizara ya Afya kubana vituo vya kutolea huduma za afya ili zisitupe taka hizo ovyo, hivyo kunusuru afya za watumiaji wa fukwe na viumbe bahari.



Taka za hospitalini zilizokusanywa na wadau wa mazingira waliofanya usafi katika ufukwe wa Rainbow, Manispaa ya Kinondoni hivi karibuni. **PICHA: JENIFER GILLA**

"Serikali kupitia maofisa afya ifanye ukaguzi katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya, wavikague na kujiridhisha wapi wanakotupa taka hatarishi za vituo vyao. Itawasaidia kuwabaini wanaotupa ovyo taka hizi.

"Hata sisi viongozi wa mitaa kwa kushirikiana na wajumbe tunapaswa kuungana na kuwa kitu kimoja kuanza doria ya kuzisaka hospitali zenye tabia hii hatarishi katika mitaa yetu," anasema.

Mmoja wa wabeba taka katika mtaa wa Makani, Anord Magori, anawatupia lawama baadhi ya wabebataka wenzake anaowaita "wenye tamaa ya fedha bila kujali madhara ya vitendo vyao", wanatumiwa na baadhi ya vituo vya afya kutupa kwenye mito taka hatarishi za hospitalini.

"Wamekuwa wanalipwa ujira wa kati ya Sh. 5,000 hadi 10,000 kwa mkupuo mmoja kutegemea na wingi wa taka hizo. Wanatupa taka hizo nyakati za usiku wakihofia kukamatwa na mamlaka za serikali," anadai Magori.

Mwandishi alizungumza na mmoja wa wanaopokea na kutupa taka hizo, mwanamume mkazi wa Kawe, Manispaa ya Kinondoni (jina tunalo). Anasema wanapokea kazi hiyo kwa tahadhari kubwa kwa kuwa wanajua wakikamatwa, adhabu yake ni kubwa ikihusiha kifungo gerezani.

Kama ilivyodokezwa na mtangulizi wake Magori, mbebataka huyo anasema mara nyingi wanakwenda kuchukua taka hizo nyakati za usiku, zikiwa tayari zimefungwa katika mifuko.

"Huwa tunatupa taka za aina hiyo kwa siri nyakati za usiku mnene. Malipo ni Sh. 5,000. Kama mzigo ni mkubwa sana, tunapewa hadi Sh. 10,000. Kuna baadhi ya vituo vya afya wanasubiri mvua ikinyesha wanazisukumizia Mto Msimbazi unaokwenda moja kwa moja baharini," anasema.

Mbebataka huyo ana angalizo lingine kwa mamlaka za kiserikali, kwamba taka hizo hazitoki katika vituo vya kutolea huduma za afya pekee, bali pia hata majumbani ambako kuna wagonjwa wanaohudumiwa wakiwa nyumbani kwa muda mrefu.

Mmoja wa wafanyakazi wa zahanati iliyoko Mbezi Beach, katika Manispaa ya Kinondoni (jina tunalo) anasema sababu kuu ya kuwapa taka hizo wabebataka wa mitaani ni kukwepa gharama alizodai "kubwa".

Mfanyakazi huyo anafafanua vituo hutakiwa kulipa Sh. 3,000 kwa kila kilo ya taka hatarishi katika hospitali za serikali wanakotakiwa kupeleka taka hizo kwa ajili ya kuteketezwa au kurejelezwa.

"Sasa unakuta una kilo 15 inakulazimu utoe Sh. 45,000. Mwenye zahanati anaona kutoa fedha hizo kila wiki ni gharama kubwa, hivyo anakutuma umpe mtu wa mkokoteni Sh. 5000 akazitupe anakojua mwenyewe, lakini huwa tunawaambia kabisa wasitupe kwenye mito iliyopo maeneo ya karibu na zahanati hii," anasema.

Daktari Bingwa Mbobezi wa Ubongo, Uti wa Mgongo na Mishipa ya Fahamu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Maxigama Ndosi, anashauri serikali kutunga sheria kali itakayozuia maduka ya dawa kuuza sindano, isipokuwa kwa wenye kibali cha daktari tu.

Mhandisi kutoka Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), Boniface Kyaruzi, anasema kuwa mwaka 1999 baraza lilianzisha Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Pwani (TCMP) kwa lengo la kulinda fukwe, mifumo ya mwambao na viumbe hai wa baharini kwa kupambana na uchafuzi wa mazingira, uharibifu wa mifumo ya ekolojia na kulinda rasilimali za bahari.

Hata hivyo, Kyaruzi anasema kuwa Licha ya NEMC kuanzisha mradi huo, ufukwe wa Rainbow unaendelea kuchafuliwa, hivyo kutoa ishara kwamba mfumo wa utekelezaji sheria una upungufu, huku kukiwa na shida nyingine ya upungufu wa miundombinu ya kuchakata taka.

Anasema NEMC inawajibika kwa mujibu wa kifungu namba 106 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004, kinachoitaka kupunguza uchafuzi wa mazingira na kuhakikisha utekelezaji wa sheria zinazohusiana na mazingira.

Kyaruzi anasema kuwa katika kuhakikisha inadhibiti utupwaji wa taka za hospitalini, serikali ilitengeneza Kanuni za Usimamizi wa Taka Ngumu (2009) zikiwamo taka hatarishi za hospitalini.

"Sheria inaelekeza kuwa uzalishaji taka unapaswa kupunguzwa kadri inavyowezekana kwa kutumia mfumo wa 'Punguza, Tumia Tena na Rejeleza (PTR)' ili kunguza kiasi cha taka kinachopelekwa kwenye madampo," Nyaruzi anasema.

Mganga Mkuu wa Manispaa ya Kinondoni, Dk. Peter Nsanya, anasema wanatekeleza miongozo iliyowekwa na Wizara ya Afya kwa kuhakikisha vituo vya kutolea huduma za afya vinakuwa na utaratibu maalumu wa kuchoma taka hizo.

Anataja moja ya mikakati hiyo ni kuhakikisha hospitali na vituo vingine vya afya ambavyo hazina kiteketezi taka, vinaingia mkataba na hospitali zenye kifaa hicho ili kupeleka taka zake huko zikachomwe kwa gharama anazoziita "nafuu".

"Kila baada ya miezi mitatu tunafanya ukaguzi katika hospitali na vituo hivyo kuangalia kama utekelezaji wa agizo hilo unafanyika ipasavyo na wale wanaokiuka kwa mara ya kwanza huwa tunawapa elimu na wakiendelea na tabia hiyo hatua za kisheria zinachukuliwa dhidi yao, ikiwamo kufungiwa kituo," anasema.

Mkaguzi wa Mazingira Manispaa ya Kinondoni, Alban Mugyabuso anasema wanayo mikakati mingi ya kukabiliana na utupwaji taka kwenye mito, lakini bado kuna watu wasio waaminifu wamekuwa wanaenenda kinyume cha maelekezo yao.

Anataja mikakati inajumuisha kutoa elimu kwa jamii kwa kushirikiana na viongozi wa serikali za mitaa kuhusu madhara ya kutupa taka na kuhimiza jamii kutoa taarifa za watu wanaokiuka taratibu za udhibiti wa taka ili wachukuliwe hatua za kisheria.

Mkaguzi Mugyabuso pia anasema wanashirikiana na maofisa afya wa manispaa kutoa elimu kwa zahanati, vituo vya afya, hospitali na maduka ya dawa katika manispaa hiyo kuhusu udhibiti wa taka hatarishi za hospitalini.

"Tuwaelekeza hospitali zinazopokea taka hizo na kuzichoma kwa bei rafiki, lakini bado zipo zahanati, vituo vya afya na hospitali zinazokwenda kinyume cha maagizo hayo kwa makusudi.

"Vilevile, kwa kushirikiana na wadau, tunafanya usafi kila mwisho wa mwezi. Wilaya pia imeweka miundombinu ya vidakia taka (trabs) kwenye Mto Feza ili kukamata taka zote kabla hazijaingia kwenye bahari. Ni teknolojia nzuri ambayo itasaidia kukabiliana na uchafuzi wa fukwe," Mugyabuso anasema.

Mwandishi alifunga safari hadi kwenye kiwanda cha Chilambo General Trade Company Limited, kampuni inayojishughulisha na kurejeleza taka na kuteketeza taka za hospitalini kilichoko Kisarawe, mkoani Pwani.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Gideon Chilamba anasema waliomba kibali cha kuteketeza taka za hospitalini kutoka Wizara ya Afya ili kusogeza huduma hiyo karibu na hospitali za eneo hilo, lakini mwamko wa wahusika bado ni mdogo.

"Tunayo mashine hapa ya kuteketeza taka za hospitalini (incinerator). Tuna leseni ya kupokea taka kutoka hospitali yoyote nchini. Uwezo tulionao ni mkubwa, lakini kazi ni chache sana, mwamko ni mdogo sana. Hata ukiangalia hospitali za hapa (Kisarawe), wengi hawana mashine hii ila sijui wanatupa wapi taka zao.

"Ninafikiri usimamizi duni wa taka za hospitalini ndiyo unasababisha haya. Hata ukienda dampo utakuta taka za hospitalini zimetupwa huko," anasema.

## Wakamatwa kwa tuhuma za wizi vifaa vya ujenzi wa shule

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WATU watatu wilayani Gairo, mkoani Morogoro wametiwa mbaroni na Jeshi la Polisi wakituhumiwa kuhusika na wizi wa nondo za ujenzi wa Shule ya Msingi ya Amali katika kijiji cha Kwipipa, kata ya Iyogwe wilayani humo.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Jabir Makame alisema jana kuwa alibaini wizi huo wakati wa ziara yake ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa wilayani humo katika kata za Iyogwe, Italagwe, Chakwale, Gairo na Rubeho.

Makame aliwataja watuhumiwa hao ni John Mbaluka, Petrol Mauji na Mnyandwa Letema ambao wanadaiwa kujihusisha na wizi wa nondo 10 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya ujenzi wa shule hiyo.

Baada ya kukamatwa, Mkuu wa Wilaya aliagiza Jeshi la Polisi kuwafikisha mahakamani watuhumiwa hao uchunguzi utakapokamilika.

"Ninataka polisi mfanye mahojiano ya kina na uchunguzi, pia kuwahoji watunza stoo na mafundi wote wanaoshukiwa na wizi huo ili kufichua mtandao mzima wa tukio hilo," aliagiza Makame.

Vilevile, Mkuu wa Wilaya aliwataka wananchi wa Kwipipa na Gairo kwa ujumla kutojihusisha na masuala ya wizi wa vifaa vya miradi ya maendeleo inayotekelezwa ndani ya wilaya hiyo kwa sababu vifaa hivyo vinanunuliwa kwa fedha zinazotokana na kodi zao.

"Ninyi wananchi ndiyo mnaopaswa kuwa na uchungu na mali hizo na ninataka hawa waliokamatwa kuwa fundisho kwa wengine," alisema Makame.

Mkuu wa Wilaya huyo pia aliwaonya makandarasi wababaishaji na wanaochelewesha kukamilisha miradi ya maendeleo katika wilaya hiyo kuwa hawatavumiliwa na watachukuliwa hatua za kisheria kwa kuhujumu miradi.

Makame alisema serikali imetoa fedha nyingi kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwenye sekta za afya, maji, elimu, barabara na nyinginezo na lengo ni kutatua changamoto za wananchi.

Akizungumzia wizi wa vifaa vya ujenzi wa shule, Mwenyekiti wa Kijiji cha Kwipipa, Herman Mshomi alikiri kutokea wizi huo kijijini kwake, akilaani kitendo hicho cha watu wachache kurudisha nyuma juhudi za serikali za kuwaletea wananchi maendeleo.

Alisema tukio hilo si la kuikomoa Serikali bali ni kujikomoa wananchi wenyewe kwa sababu miradi inayoletwa na serikali hainufaishi serikali, bali wananchi wenyewe na hivyo wanapaswa kuwa walinzi namba moja wa miradi hiyo.

# Malasusa ataja kiini ndoa nyingi kuvunjika

## ▪Akemea watoto kugeuzwa bidhaa

**Na Christina Haule,** MWANZA

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Alex Malasusa ameitaka jamii kusimamia maadili ya malezi na ulinzi kwa mtoto ili kumwepusha na ndoa za utotoni zinazochangia talaka nyingi kwa wanandoa nchini.

Askofu Dk. Malasusa alisema hayo jana jijini Mwanza wakati akifungua mafunzo ya siku tatu kwa waandishi wa habari kutoka vyombo mbalimbali vya habari nchini yaliyoandaliwa na KKKT kupitia Upendo Media chini ya mradi wa Hapana Marefu Yasiyokuwa na Mwisho.

Alisema ndoa za utotoni zinaondoa upendo kwa binadamu na ndio maana kuna tatizo kubwa la talaka nchini na hiyo ni kuonesha kuwa mmoja wa wanandoa hakuwa na uamuzi wa kuingia katika ndoa.

"Watoto wengi wanasukumwa katika ndoa huku wakiwa hawana uhuru wa kuingia huko na ndio maana kunakuwa na talaka nyingi kwa wanandoa kwa sasa," alisema Askofu Dk. Malasusa.

Alisema ana imani kuwa Tanzania imefaulu kwenye mambo mengi na hata hili wanahabari wakilichukulia kwa undani litakomeshwa.

Alisema wapo baadhi ya wazazi wanaokatisha ndoto za watoto wao kwa kuwaachisha masomo na wengine kuwalazimisha kufanya vibaya kwenye masomo ili waozeshwe, hivyo kuitaka jamii kusimamia na kuisaidia serikali kudhibiti kitendo hivyo.

Kiongozi huyo wa kiroho alisema wazazi wamekuwa wanaamua kujipatia umiliki wa mtoto, hasa pale wanapoona anapewa ubini wake, hivyo kuamua kumtumia watakavyo isivyo sahihi.

"Wengine wanaamua kumwuza kwa mahari kabla ya umri. Tuondoe fikra za watoto kuwa bidhaa, hawapo kwa ajili ya kuuzwa, tusimame pamoja kukemea vitendo hivi," alisema Dk. Malasusa.

Alisema watoto wanatakiwa kufunzwa juu ya haki zao wanazopaswa kuzisimamia na kujitetea kwa kujua kuwa wao wana maisha zaidi kuliko kukimbilia katika ndoa.

Mkurugenzi wa Upendo Media, Neng'ida Johannes alisema tatizo la ndoa za utotoni ni kubwa katika mikoa ya Dodoma, Shinyanga, Tabora, Mara na Lindi.

Aliwahimiza waandishi wa habari kuendelea kusemea maeneo yaliyoathirika ili kusaidia watanzania kuacha tabia za kuoza watoto wadogo.

Msimamizi Mkuu wa Programu ya Maisha Endelevu na Uwezeshaji kutoka KKKT, Patricia Mwaikenda, alisema ni wakati sasa jamii kutambua namba ya serikali 116 ili kutoa taarifa wanapobaini ukatili wa aina yoyote.

Mwaikenda alisema mradi huo unatekelezwa katika mikoa minne, ikiwamo ya Zanzibar na kupata wakufunzi 30 ukiwa na mitaala inayosimamia na vyuo vikuu vinne nchini sambamba na mafunzo kwa walimu 24 wa shule za awali mkoani Morogoro.

Alisema tangu mradi uanze mwaka 2023, mpaka sasa kanisa tayari limeshaokoa watoto watatu waliokuwa wanaozeshwa katika umri mdogo ambao hadi sasa wana mafanikio kielimu.



**Msimamizi Mkuu wa Programu ya Maisha Endelevu na Uwezeshaji kutoka KKKT, Patricia Mwaikenda, alisema ni wakati sasa jamii kutambua namba ya serikali 116 ili kutoa taarifa wanapobaini ukatili wa aina yoyote.**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**TANGAZO LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA MTWARA, LINDI NA RUVUMA KATIKA HALMASHAURI ZA WILAYA ZA MADABA, NAMTUMBO NA TUNDURU.**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza unafanyika katika Mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma katika Halmashauri za Wilaya za Madaba, Namtumbo na Tunduru tarehe 28 Januari hadi 03 Februari, 2025. Zoezi la uboreshaji wa Daftari linafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. **SIKU:** Uboreshaji utafanyika kuanzia siku ya Jumanne tarehe 28 Januari hadi siku Jumatatu tarehe 03 Februari, 2025
2. **VITUO:** Uboreshaji utafanyika katika vituo vilivyomo katika Mitaa, vijiji na vitongoji
3. **MUDA:** Vituo vitafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni

**Uboreshaji utahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa miaka 18 na zaidi ambao hawakuwahi kuandikishwa hapo awali, na ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka
2. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi (Jimbo au Shehia).
3. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
4. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
5. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili kwa pamoja, wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume ***www.inec.go.tz*** au anuani ya ***ovrs.inec.go.tz*** kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la shehia anayokusudia kuhamia, kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo katika kituo cha kuandikisha Wapiga Kura ili kukamilisha taratibu na kupatiwa kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo (maarufu kama kitochi au kiswaswadu) anaweza kuingia kwenye mfumo wa OVRS kwa kupiga *152*00#, kisha, atachagua namba 8 na kubonyeza, kisha atachagua namba 2, kisha atabonyeza namba 3 hapo atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga simu namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali na hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

***KUJIANDISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA***

**Limetolewa leo tarehe 20 Januari, 2024 na:**

**Christina P. Ballali**
**KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Malezi bora ya mjamzito yazingatiwe kulinda afya ya mama na mtoto

**UKUAJI** wa mtoto kibaiolojia huanza kuhesabiwa tangu siku ya kwanza mimba inapotungwa. Wataalamu wa afya wanazitaja siku 1,000 za ukuaji huo kuwa muhimu zaidi kwa afya ya mama na mtoto.

Wiki 36 na kuendelea kwa ujauzito zimo katika siku 1,000 zinazotajwa kuwa muhimu katika ukuaji wa mtoto tangu tumboni mwa mama hadi anapofikisha umri wa miaka miwili.

Inapotokea tofauti katika ukuaji huo, ikiwamo mama kuathiriwa na mazingira yanayomzunguka kiuchumi na kijamii, athari huwa kwa mama na mtoto moja kwa moja.

Magonjwa ya akili kama vile sonona, ni miongoni mwa changamoto ambazo baadhi ya wajawazito na mama aliyetoka kujifungua hukumbana nayo na kuathiri ukuaji wa mtoto kiafya.

Kama ilivyoelezwa na wasaikolojia tiba kutoka Hospitali ya Saifee, mkoani Dar es Salaam, elimu ya afya ya akili kwa mama kabla na baada ya kujifungua, hupunguza madhara yatokanayo na sonona.

Wataalamu hao wanasema athari za sonona kipindi cha ujauzito na baada ya mama kujifungua zisipotibiwa mapema, huathiri mtoto aliyeko tumboni na akishazaliwa husababisha mtoto kuwa na uhusiano duni kijamii.

Kwa mujibu wa wataalam hao, sonona kwa mjamzito huvunja muunganiko wa mapenzi kati ya mama na mtoto. Muunganiko wa kihisia na kimwili ambao huanza wakati wa ujauzito na kuendelea katika maisha ya mtoto, wanautaja ni muhimu ili jamii kuwa na kizazi kilicho na upendo, weledi na matokeo chanya.

Mabadiliko ya homoni kwa kipindi cha ujauzito, kama ilivyoelezwa na wataalamu hao kwa Nipashe, ni jambo la kawaida kwa mjamzito, ingawa yakichukua muda mrefu humwathiri yeye na kiumbe kilichomo tumboni.

Kuna angalizo lingine -- sonona huonekana kwa dalili tofauti kwa kipindi cha wiki mbili, kama vile mtu kukata tamaa, kukosa usingizi ama kulala kupitiliza, kushtuka usingizini, kula zaidi au kula kidogo. Wengi wa wanaougua, chanzo kikuu ni ugomvi kati ya mtu au jamii inayomzunguka kwa muda mrefu.

Lipo angalizo lingine linalotia simanzi kutoka kwa wataalam --duniani asilimia 60 ya wajawazito hupitia sonona. Faraja pekee iliyopo ni kwamba ugonjwa huo unatibika kwa elimu ya saikolojia tiba au dawa.

Nipashe tunaungana na wataalam hao kuitaka jamii kuchukua hatua kukabiliana na sonona kwa wajawazito, ikizingatiwa takwimu zinaonesha mmoja kati ya kinamama saba hukumbwa na tatizo hilo.

Huzuni kupitiliza, kukosa hamu ya kula, kupungua au kuongezeka uzito na hofu, hasa hofu pale muda wa kujifungua unapokaribia, vinatajwa na wataalam kuwa hatari zaidi kwa afya ya akili.


Kwa mujibu wa wataalam hao, mtoto akizaliwa na mama mwenye shida hiyo, atakosa muunganiko kwa jamii, atakosa uhusiano wa kijamii, atachelewa kukua na kusumbuliwa.

Hivyo, ni muhimu jamii ikumbatie malezi bora kwa mjamzito na baada ya kujifungua, vyote vikitajwa na wataalam huwa chachu ya afya kiakili kwa mama, mtoto na jamii kwa kuwa maandalizi ya ukuaji wa mtoto huanza tangu siku ya kwanza mimba ilipotungwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Dira isiwasahau wanaolala mitaani

Na Tuntule Swebe

**IMEZOELEKA** miji na majiji makubwa kama Dar-es Salaam ni maeneo ya kutafuta maisha hivyo watu walio wengi wanatoka vijijini kupata maisha bora.

Wapo baadhi wanaingia mijini bila kuwa na ndugu wala mipango au fedha mfukoni za kuanza maisha mapya mjini.

Hivyo, wanalazimika kuingia mtaani na kufanya shughuli zao lakini wanalala nje kama vile chini ya madaraja mfano Ubungo, Kimara, TAZARA kwa Dar es Salaam.

Wapo wanaojisitiri kando ya barabara, nje ya vibanda vya biashara na maduka, pembezoni mwa nyumba za watu na kwenye masoko.

Wasaka maisha hawa wengine wanatuhumiwa kuwa wahalifu kuhusishwa na kuwaibia watu na wakati mwingine wanajeruhi na kupora.

Moja ya wajumbe wa serikali za mitaa kutoka Kisutu Dar-es Salaam, anaeleza kuwa mwaka 2024 watu wanaolala nje ni chanzo cha wizi kwani hawana cha kufanya.

Japo siyo wote ni baadhi lakini kutoka vijijini wanakuja mijini bila msaada, kazi wala fedha kunaweza kuwafundisha uhalifu.

Licha ya kwamba wizi ni tabia ya mtu binafsi anayoweza kutoka nayo kwao umaskini na kukosa chakula kunawapa mawazo na maamuzi ya kufanya chochote ili kupata riziki na chakula.

Uhalifu wanaojihusisha nao ni pamoja na kuvuta bangi, kutumia mihadarati na kupora mali za watu kama simu, pochi na hata pikipiki.

Pamoja na uhalifu pia ni chanzo cha uchafu mijini kwani hawana mahali rasmi pa kulala, kujisaidia na kupata huduma kama maji ya kuoga, kufua nguo na hivyo kujihudumia popote.

Wanaweza kufua mtoni, kupasua mabomba kupata maji, kwenda kwenye gereji hivyo kuchangia kuongeza taka na mazingira machafu mijini kwa kuwa hata wakila hutupa mabaki na vifungashio popote.

Kukosa huduma hizo kunachangia kujisaidia haja ndogo kwenye kuta za uzio, kutumia mifuko kujisaidia na kusababisha vinyesi kuzagaa huku baadhi wakitumia chupa za maji kwa ajili ya haja ndogo.

Tanzania ni nchi inayolenga kufikia kiwango cha juu cha awajibika kuchukua hatua kukabiliana na hali duni ya vijana.

Kama lengo la Dira ya Maendeleo ya 2050 ni kuwa na maisha bora kwa kila Mtanzania isiwapuuze vijana kama hao na mchango wao.

Ikumbukwe kama nchi inawasahau vijana inaweza kujiweka katika hatari kubwa ya kukwama kimaendeleo, kutishia usalama na maadili kwa sababu ya kuwa na kundi kubwa la wahalifu ambao ni vijana wenye umri mdogo.

Katika dunia ya sasa na hata ndani ya siku zijazo za dira ya maendeleo ya 2050 kama nchi haitawekeza katika miradi ya kuinua maisha ya vijana hawatakuwa na nafasi ya kushindana na mataifa mengine katika sekta mbalimbali ili kufikia maendeleo endelevu.

Tanzania ina nafasi ya kujiandaa na kuimarisha maisha ya vijana kuanzia kiuchumi ikiwa itawekeza kikamilifu mikakati kwa kurejea sensa ya watu na makazi ambayo inasema vijana ni karibu nusu ya raia wa nchi hii.

Serikali ikumbuke vijana hawa ndiyo nguzo ya maendeleo ya nchi hii na lazima ifanye juu chini kuweka mikakati, mipango na sera madhubuti za kuboresha maisha yao, kwani ikitetereka na kuwaacha wajirundike mijini itakuwa imeweka msingi mbaya na kukwamisha dira ya maendeleo ya 2050.

Cha msingi ni kuwapatia elimu inayoendana na mabadiliko ya dunia ya kidijitali, kielektroniki na inayojaa ubunifu. Serikali ifanye hivyo kupitia mfumo mpya wa masomo wa kufundisha elimu ya amali, uanagenzi na kuhitaji kuwekeza zaidi katika teknolojia ili kufanikisha mitaala inayobadili maisha ya vijana.

Bila teknolojia, ubora wa elimu ambayo inapaswa kuwaandaa vijana kwa ujenzi wa taifa lao itakuwa vigumu kufanikisha dira 2050.

Lakini serikali ikumbuke kuwa kuwaelimisha watoto, vijana na Watanzania bila kuwapatia kazi ni kuongeza matatizo katika nchi ni lazima kujenga viwanda vidogo na vikubwa vijijini kutoa ajira.

HABARI KITAIFA

# Mkandarasi mradi wa maji abanwa

**Na Said Hamdani,** LINDI

NAIBU Waziri wa Maji, Kundo Methew amemtaka mkandarasi aliyepewa kazi ya ujenzi wa mradi wa maji wilayani Kilwa, mkoani Lindi, kukamilisha kazi ndani ya muda aliopangiwa ili kuwawezesha wananchi kuondokana na tatizo la kukosa huduma hiyo muhimu.

Kundo alitoa agizo hilo jana alipozungumza na viongozi, watendaji walio chini ya wizara hiyo na mkandarasi huyo baada ya kumaliza kukagua na kuona utekelezaji unavyoendelea wilayani Kilwa.

Mradi huo wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 18 (Sh. bilioni 44) unatekelezwa na Mkandarasi AFCONS wa jijini Dar es Salaam.

Naibu Waziri Kundo akizungumza na viongozi na watendaji hao, alisema mradi huo ulitakiwa kukamilika mapema mwaka jana, lakini kutokana na changamoto zilizojitokeza, kikiwamo Kimbunga Hidaya, walilazimika kuongeza muda hadi Septemba mwaka huu.

Alimtaka mkandarasi huyo kuongeza kasi ya utekelezaji pamoja na idadi ya wafanyakazi ili kazi ikamilishwe ndani ya muda uliopangwa kwa ajili ya kuwaondolea wananchi kikwazo katika upatikanaji huduma hiyo muhimu.

Naibu Waziri huyo alisema Kimbunga Hidaya kisiwe sababu ya kuchelewesha kukamilisha maendeleo ya mradi husika, hivyo ifikapo mwezi Juni mwaka huu, kazi ya ulazaji mabomba ikamilike.

"Mkandarasi unalazimika kuongeza kasi na idadi ya wafanyakazi usiku na mchana ili jamii ipate maji," alisisitiza Naibu Waziri Kundo.

Pia alisisitiza ifikapo mwezi Septemba mwaka huu, kazi ya ujenzi iwe imekamilika na wananchi wapate huduma ya maji safi na salama kwa matumizi ya binadamu.

Mkandarasi AFCONS alipokea maelekezo hayo na kumhakikishia Naibu Waziri huyo kwamba atamaliza kazi aliyopewa ndani ya muda alioongezwa na si zaidi ya hapo.

Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Mohamedi Nyundo alishukuru serikali kuupatia mradi huo fedha nyingi na kumhakikishia Naibu Waziri huyo kuwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya itakuwa anafuatilia utendaji kazi wake kwa karibu zaidi.

Nyundo alisema mradi huo unaojengwa kutokea chanzo cha kijiji cha Mavuji, utakapokamilika utanufaisha wananchi 59,900 katika miji midogo ya Kivinje, Masoko pamoja na vijiji vya Nangurukuru, Mchakama na Mavuji yenyewe.



Naibu Mkuu wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Taaluma, Utafiti na Ushauri wa kitaalam, Prof. Ezekiel Amri, akizungumza wakati akifungua mafunzo ya siku tano kwa wakufunzi wa taasisi hiyo, jijini Dar es Salaam jana, yenye lengo la kuwajengea uwezo katika ufundishaji kuendana na mabadiliko ya teknolojia. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mapya yaibuka kifo cha mwandishi

**Na Samson Chacha,** TARIME

KIFO cha aliyekuwa mwandishi wa habari wa kampuni za The Guardian Ltd na Mwananchi Communication Ltd kwa nyakati tofauti, Charles Mwita (48) kimeibua mambo mapya.

Ufuatiliaji wa Nipashe umebaini Mwita aliuawa kwa kupigwa risasi kifuani akiwa nchi jirani Kenya.

Mwandishi huyo aliripotiwa kuuawa wiki iliyopita kwa kupigwa risasi na watu wasiojulikana wilayani Tarime, mkoani Mara.

Hata hivyo, taarifa za mauaji hayo kufanyika katika kata ya Sirari, Tarime zilikanushwa na Jeshi la Polisi kupitia taarifa iliyotolewa Januari 17 mwaka huu na Msemaji wa Jeshi hilo Makao Makuu Dodoma, DCP David Misime, likisisitiza hakuna tukio la namna hiyo nchini.

Kufuatia hali hiyo, Nipashe imefuatilia kwa undani suala hilo hata kuvuka mipaka ya nchi hadi Kenya katika eneo la Gwikonge na kubaini ndiko tukio hilo lilitokea huko ambako kiongozi wa eneo hilo 'Sub Chief' Bisare Sagamo alithibitisha hilo mwishoni mwa wiki.

Katika mazungumzo na Nipashe, Sagamo alieleza kusikitishwa na tukio hilo na kueleza kuwa kijana huyo alipigwa risasi alizodai "zaidi ya mbili" kifuani na watu wasiojulikana.

"Tumesikitishwa na mauaji ya kijana huyu yaliyotekelezwa usiku nyumbani kwao. Huyu kijana alikuwa Dar es Salaam akifanya kazi ya uandishi wa habari. Alifika hapa kijijini Ikerege 'Location' ya Gwikonge hivi karibuni na kulikuwa na migogoro imejitokeza ya kugombea ardhi na mashamba aliyoacha baba yao," alidai.

Alidai kuwa baba yao, Mwita Nyagakende, kabla ya kifo chake, alikuwa Mbunge wa Jimbo la Kurya West, mkoa wa Nyanza , aliwaachia mashamba ambayo kwa Kenya yanatajwa kuwa na thamani kubwa na kuwa huenda kifo cha kijana huyo kimetokana na migogoro ya ardhi waliyokuwa nayo.

"Kwetu hapa ardhi ina thamani kubwa kama dhahabu na inadhaniwa inaweza kuwa chanzo cha mauaji japo kuwa bado uchunguzi unaendelea kuwabaini wahusika," alisema Sagamo.

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Tarime/Rorya, Michael Njera alisema kuwa baada ya kuona taarifa hizo zinasambaa zikitaja kijana huyo kuuawa katika mji wa Sirari, tarafa ya Inchugu, wilayani Tarime, walifuatilia na kubaini si za kweli.

Alisema ukweli ni kuwa aliuawa kwa kupigwa risasi nyumbani kwao kijijini Ikerege, barabara ya kwenda Kehancha, wilaya ya Kurya, Kenya.

"Kwanza tunakanusha taarifa zilizoandikwa na moja ya gazeti siku ya Jumamosi zilizodai mwandishi huyo kuuawa wilayani hapa kwani hatukuwa na taarifa yoyote iliyoripotiwa kwenye vituo vyetu vyote vya polisi juu ya mauaji hayo," alisema Kamanda Njera.


Alisema kuwa baada ya kufuatilia na kufanya uchunguzi kwa kushirikiana na majirani Kenya, Jeshi la Polisi la Kenya lilipata taarifa sahihi kuwa mwandishi huyo aliuawa katika kijiji cha Ikerege nyumbani kwao, kilomita 10 kutoka mji wa Isebania, barabara ya kwenda Kihancha.

Kamanda Njera alisema mauaji hayo yalifanyika usiku kwa kupigwa risasi na watu wasiojulikana na mwili wake uko kwao Kenya kwa taratibu za kiuchunguzi.

"Tunawatahadharisha watu, akiwamo mdogo wa marehemu, Nelson Mwita na wanamitandao kufanya utafiti wa kina kuhusu habari wanazotoa kabla ya kuzisambaza kwenye vyombo vingine na kuleta taharuki kwa jamii," alisema Kamanda Njera.

KABWELA

FADHILI MOHAMED





Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani akikagua lori lenye namba za usajili T 139 DRP, lililomshinda dereva na kupinduka baada ya kuyagonga magari matatu na bajaji nne katika mteremko wa barabara ya Wazo, eneo la Msikitini, kata ya Wazo, Dar es Salaam jana. Wananchi wamelalamikia kuwa barabara hiyo ni nyembamba licha ya kuwa inatumiwa na magari madogo na malori makubwa yanayobeba saruji kutoka kiwandani. Baadhi ya watu walijeruhiwa katika ajali hiyo. **PICHA: JOHN BADI**

# Atiwa mbaroni kwa tuhuma kutengeneza picha za utupu

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani linamshikilia mtu mmoja anayedaiwa kutengeneza picha mjongeo za utupu zenye maudhui machafu na kuzisambaza huku akiziunganisha na majengo, mazingira ya Shule ya Sekondari Baobab iliyoko Mapinga, wilayani Bagamoyo.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake mjini Kibaha jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Salim Morcase alisema picha hizo zisizo na maadili zilitengenezwa na kuunganishwa na baadhi ya majengo ya shule hiyo ili kuaminisha umma kuwa vitendo hivyo vinafanywa na wanafunzi wa shule hiyo.

Akielezea tukio hilo, Kamanda Morcase alisema kuwa Januari 3 mwaka huu walipokea taarifa kutoka kwa uongozi wa Shule ya Baobab wakielezea kutengenezwa kwa picha mjongeo za utupu zenye maudhui machafu na kusambazwa katika mitandao ya kijamii kinyume cha sheria za nchi.

"Jeshi la Polisi Mkoa wa Pwani limefanya uchunguzi na limefanikiwa kumkamata mtu mmoja ambaye uchunguzi wa kitaalamu ulisaidia kufikia na kumkuta na picha hizo na kifaa cha kieletroniki ambacho alikuwa anatumia kusambaza picha hizo chafu," alisema. Kamanda huyo pia alisema kuwa jeshi hilo linaendelea kuwasaka watu wengine waliohusika katika kutengeneza na kusambaza picha hizo mjongeo.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Shajar inayomiliki Shule ya Sekondari Baobab, Shani Swai akielezea kuhusiana na tukio hilo, alisema picha hizo mjongeo zilianza kusambazwa Desemba 31, 2024 na kwamba taharuki iliibuka kwa wafanyakazi pamoja na wazazi.

"Wazazi walipata taharuki, wengi walipiga simu tukawaelekeza wawe watulivu kwa kuwa wakati hizo picha zinasambazwa wanafunzi walikuwa likizo, kilikuwa kipindi cha mpito wetu, taasisi na wafanyakazi," alisema.

Swai alisema kwa kuwa hawana ujuzi wa kuchunguza picha hizo, waliamua kutoa taarifa polisi ili zifanyiwe kazi na kuwasaka waliohusika kutengeneza picha hizo.

"Picha zilizosambaa ni za aina mbili, walidukua picha za wanafunzi wakiwa kwenye mahafali, hizo ni sawa wanaonekana wakiwa kwenye mavazi ya heshima, lakini hizi nyingine za utupu walizotengeneza siyo za kwetu, wanafunzi wetu hawahusiki hapo," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Taaluma ya Shule hiyo, Fredy Ntevi, alisema picha chafu zilizosambazwa zinaonesha wanafunzi wakiwa wamesuka nywele za kutengeneza, jambo ambalo ni tofauti kwa kuwa wanafunzi wa shule hiyo wanasuka aina moja ya nywele za asili, maarufu twende kilioni.

Ntevi alisema wanaamini serikali ina wataalamu wengi ambao wanaweza kushughulikia tatizo hilo ambalo limeichafua taasisi yao kwa kuonesha picha chafu tofauti na watoto wao ambao muda wote wanavaa mavazi ya heshima na wana nidhamu.

Makamu Mkuu wa Shule Taaluma, Alphonce Kamisa alisema pamoja na taharuki hiyo, kutokana na wazazi wengi kuzifahamu zaidi shule hiyo wameendelea kuwarudisha watoto kuendelea na mwaka mwingine wa masomo.

Alisema kati ya wanafunzi zaidi ya 1,700, hadi sasa ni wanafunzi 1,600 ambao tayari wameripoti na ambao hawajaripoti, wazazi wao wametoa sababu za msingi, walipiga simu kuomba watoto wao kuchelewa kufika.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
Tarehe: 20/1/2025

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Jumatano** tarehe **21-1-2025** kampuni ya **HAINAN INTERNATIONAL LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka Nyerere National Park kuelekea **DAR ES SALAAM** Mloganzila, gari hilo lenye namba za usajili: **T 176 DFN / T 171 DFN.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **18.00** |
| **Upana** | - | **mita** | **3** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5** |

3. Njia itakayotumika: Nyerere National Park hadi **DAR ES SALAAM Mloganzila** kupitia **Mloka-Kibiti Road, Kilwa&Morogoro ROAD.** Gari itasafiri muda wa mchana tu ***(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)***

118332902

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

## UGENI MIKOA SITA

# Kampeni Msaada wa Kisheria ya Mama Samia kuanza wiki hii

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMPENI ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia inatarajiwa kuzinduliwa Januari 24 mwaka huu katika mikoa sita, ikianzia Kigoma, Katavi, Tabora na Mtwara.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma.

Alisema katika kutekeleza kampeni hiyo, wizara imepanga kuifikia mikoa sita ambayo ni Kigoma, Kilimanjaro, Geita, Katavi, Tabora na Mtwara na kuzifikia kata 10 kwa kila halmashauri za mikoa tajwa.

Dk. Ndumbaro alisema timu za wataalamu katika sekta ya sheria zitaweka kambi kwa muda wa siku tisa katika mikoa hiyo na huduma za msaada wa kisheria zitatolewa bila malipo.

Alisema kuwa tarehe 25 Januari, kampeni hiyo itazinduliwa katika mkoa wa Geita na baadaye tarehe 29 itazinduliwa katika mkoa wa Kilimanjaro na kwamba uzinduzi huo utafuatiwa na utolewaji huduma za msaada wa kisheria kwa siku tisa katika maeneo hayo na kuzifikia halmashauri zote za mikoa sita.

"Nitoe rai kwa wananchi wote kujitokeza kwa wingi kupata huduma za msaada wa kisheria wakati wote wa kampeni.

"Katika kipindi cha utekelezaji kampeni, timu ya wataalam zitakuwa uwandani katika halmashauri zenu na niwaombe mfuatilie matangazo ya vyombo vya habari na uongozi wa mitaa ili kufahamu sehemu ambazo watoa huduma watakapokuwa," alisema Dk. Ndumbaro.

Alisema sambamba na utekelezaji Kampeni ya Msaada wa Kisheria, wizara kupitia Idara ya Katiba na Ufuatiliaji Haki, itakuwa inafanya mafunzo kwa kamati za usalama katika ngazi ya mikoa na wilaya.

Alisema kuwa pia watawajengea uwezo wataalam wa halmashauri na watendaji kata kuhusu elimu ya uraia na utawala bora, lengo ikiwa ni kuwawezesha katika utekelezaji majukumu yao ya kazi kwa ufanisi na kufuata sheria, kanuni na taratibu.

"Ninapomaliza taarifa hii, ninawashukuru sana kwa kuendelea kushirikiana na wizara katika kutoa habari za shughuli zinazofanywa na wizara ikiwamo utekelezaji Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia.

"Niwaombe mara baada ya kumaliza mkutano huu tufikishe habari hizi kwa wananchi ili waweze kuitumia Kampeni ya Msaada wa Kisheria katika kusuluhisha migogoro inayojitokeza na kupata suluhu," alisema.

Waziri huyo alisema Wizara ya Katiba na Sheria katika kuweka mwendelezo wa utatuzi wa migogoro hata baada ya kumalizika kwa kampeni hiyo, imeanzisha madawati ya msaada wa kisheria yanayopatikana katika halmashauri zote nchini ambayo yanatoa msaada wa kisheria bila malipo.

Dk. Ndumbaro pia alisema yapo mashirika yanayotoa msaada wa kisheria yenye mawakili, wanasheria na wasaidizi wa kisheria nchi nzima ambayo nayo majukumu yao ni kuhakikisha wananchi wanasikilizwa na kupatiwa huduma za msaada wa kisheria ili haki itendeke kwa kila mwananchi mwenye uhitaji.



## Wanachama ushirika sasa kupata taarifa kidigitali

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

MRAJIS wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Nchini (TCDC), Dk. Benson Ndiege amesema zaidi ya watoa huduma 30 katika sekta ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), wamekubali kuanza kushirikiana na serikali kuwasaidia wanachama wa vyama hivyo kupata huduma na taarifa za vyama vyao.

Akizungumza na Nipashe jana kuhusu mpango huo wa ushirika kidijitali, Mrajis huyo, alisema lengo la serikali ni kuongeza thamani katika ushirika.

Alisema kupitia Kampeni ya 'Ushirika Kidigitali' inayoendeshwa na TCDC, itatolewa elimu kuhusu ushirika na uwekezaji unaofanywa na vyama hivyo.

Dk. Ndiege, amewasihi wanachama wa vyama hivyo na wananchi kufuatilia kampeni hiyo ili kujifunza mambo mbalimbali yanayofanywa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania kuboresha sekta ya ushirika nchini.

"Tumekuja na Mfumo wa Kidigitali wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU), kama serikali ili kuhakikisha tunakuwa na ushirika imara. Kwa hiyo lengo kubwa la MUVU ni kuongeza uwazi kwenye utendaji wa shughuli za ushirika.

MUVU itatambua wanaushirika wote kwa maana ya mmoja mmoja, vyama na mali zote za vyama vya ushirika.

Watoa Huduma katika Vyama Vya Ushirika, ni vyema wakahakikisha mifumo yao inaunganishwa na MUVU."

# Ofisa Misitu kizimbani kwa kupokea rushwa

**Na Jaliwason Jasson,** KITETO

OFISA Misitu wa Jumuiya ya Uhifadhi wa Msitu wa Suledo uliopo Wilaya ya Kiteto mkoani Manyara, Siloma Mtero, amefikishwa mahakamani akikabiliwa na tuhuma za kupokea rushwa ya Sh. 600,000.

Mshtakiwa huyo alifikishwa katika Mahakama ya Wilaya hiyo jana na kudaiwa kuomba na kupokea kiasi hicho cha fedha kutoka kwa Mwenyekiti wa Serikali ya Kitongoji cha Ndilali.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Yahaya Masakilija alidai kuwa mshtakiwa huyo aliomba rushwa hiyo ili awaruhusu baadhi ya wakazi wa kitongoji hicho kufanya shughuli za kilimo ndani ya msitu huo.

Kesi hiyo namba tatu ya mwaka huu, inasikilizwa na Hakimu wa Mahakama ya Wilaya ya Kiteto, Aron Losioki.

Kwa mujibu wa hati hiyo ya mashtaka, mshtakiwa huo anadaiwa kukiuka kifungu cha 15 (1) (a) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329 ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

Pia, mshtakiwa huyo anakabiliwa na tuhuma nyingine za kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, kinyume na kifungu cha 302 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 kama iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

Mshtakiwa huyo alikana mashtaka yote yanayomkabili.

Baada ya mshtakiwa huyo kukana mashtaka, Hakimu Losioki, alitoa masharti ya dhamana, lakini alishindwa kutimiza na kuamuru kupelekwa mahabusu.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Januari 28, mwaka huu, itakapotajwa tena mahakamani hapo.



Mganga Mkuu wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Dk. Fani Mussa akizumgumza wilayani humo jana, wakati wa uzinduzi wa kampeni harakishi ya siku sita ya uibuaji wa wagonjwa wa kifua kikuu kwenye jamii iliyoanza Januari 17 hadi 24 Mwaka huu katika Kituo cha Afya cha Ubwari. Wengine ni Mratibu wa Kifua Kikuu na UKIMWI, Ester Minja (kushoto), Katibu wa Afya wa wilaya, Cecilia Muna (wa pili kushoto) na (kulia) ni Mratibu wa Elimu ya Afya kwa umma, Shabani Seif. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Majaji, mahakimu wanawake kutokomeza ukatili wa kijinsia

**Na Allan Isaack,** ARUSHA

CHAMA cha Majaji na Mahakimu Wanawake Tanzania (TAWJA), kimepanga kufungua klabu za kupambana na matukio ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake, watoto na makundi maalumu katika shule sita za sekondari mkoani hapa.

Hayo yamo katika hotuba ya Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania (TWPG), Shally Raymond, aliyemwakilisha Spika wa Bunge, Dk.Tulia Akson katika Kongamano la Miaka 25 ya TAWJA.

Shally, alisema klabu hizo zitaanzishwa katika shule za sekondari za Ilboru, Arusha, Kimandolu, Kaloleni, Muriet na Sinoni kwa ajili ya kutoa elimu ya utambuzi wa matukio dhidi ya makundi hayo.

Alisema chama hicho kimejipambanua kupambana na mila kandamizi, ndoa za utotoni na ukeketaji wa wanawake kwa kuwa nafasi za uongozi na maamuzi bado ni kikwazo katika kufikia usawa wa kijinsia.

"Mila na tamaduni potofu ni changamoto kubwa inayosababisha kufifisha ndoto za wanawake katika kujiletea maendeleo ya kweli japokuiwa mbinu za pomaja na juhudi za kujikwamua katika madhila hayo zinafanyika ili kubomoa mifumo kandamizi na kuvunja minyororo iliyojikita kwenye jamii kwa kipindi kirefu," alisema.

Alisema maadhimish hayo ni tukio linalostahili kushereheke-wa kwa kuwa dhima ya chama hicho ni kuwa mshumaa wa mwanga na matumaini kwa kupigania haki za kijinsia ikiwamo za wanawake na watoto.

Alisema bado wananwake na watoto wako nyuma katika kulinda na kutetea haki zao za msingi kulingana na mila na desturi na mifumo dume iliyoko katika jamii.

Pia, alisema endapo wanaume watashiriki kwenye mapambano dhidi ya matukio hayo itakuwa ni nyenzo muhimu kubadilisha fikra na mitizamo hasi dhidi ya wanawake na watoto.

Alisema mabadiliko wanayotafuta yanamgusa kila mwananchi katika harakati za kuvunja mifumo kandamizi ambayo imekuwa ikizidi kukithiri katika jamii.

"Pamoja na ukweli kuwa mabadiliko siyo jambo rahisi kupokewa, sauti zetu na mikakati ni kitu muhimu ili kufikisha ujumbe sahihi," alisema Shally.


Mwenyekiti wa TAWJA, Barke Sehel, alisema katika maadhimisho hayo, wamejipanga kuunganisha nguvu kupinga matukio hayo dhidi ya wanawake na watoto.

Barke, alisema kuelekea maadhimisho hayo yenye kaulimbinu ni 'Kusherekea utofauti na mshikamano katika usawama wa kijinsia', wamejipanga kutoa elimu, kuhamasisha na kuunda uelewa wa pamoja katika haki za kijinsia na hatua za kuchukua dhidi ya watu wanaojihusisha na matukio hayo ili yasiendelee kuathiri jamii.

"Dhamira yetu ya kudumisha haki na usawa wa kijinsia imejikita zaidi katika kutetea na kukuza haki za wanawake,watoto na makundi maalum hapa nchini," alisema Barke na kuongeza kuwa:

"Mheshimiwa mgeni rasmi, wanachama wa TAWJA tutapata muda wa kutembelea shule za sekondari sita kwa ajili ya kuanzisha klabu za haki za kijinsia shuleni."

Vilevile, alisema wanachama watakaotembelea shule hizo, watatoa elimu kwa wanafunzi kuhusu namna ya kutambua aina zote za vitendo hivyo na sehemu za kwenda kutoa taarifa kama vimetendeka, elimu ya kujiwekea malengo na kujali afya zao.



# Kikongwe aliyetelekezewa pacha apata wasamaria

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAKUNDI sogozi mawili ya 'WhatsApp' wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga yamechangisha zaidi ya Sh.milioni mbili na kutoa mahitaji kwa Kashindye Mhoja (64) watoto pacha wa mwezi mmoja baada ya kutelekezwa na baba yao ili kumsaidia kuwatunza.

Hivi karibuni Nipashe iliripoti habari kuhusu Kashindye, Mkazi wa Kata ya Mwendakulima Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, kutelekezewa mapacha hao na mkwewe (35) baada ya mama yao kufa kwa kuishiwa damu mwezi mmoja baada ya kujifungua.

Akikabidhi mahitaji hayo juzi, mwanzilishi wa makundi hayo ya Kahama News na Siasa, William Bundala, alisema wamehamasishana kuchanga fedha baada ya kuguswa na tukio la mapacha hao kutelekezwa na baba yao bila msaada wowote na kutokomea kusikojulikana.

Bundala alitaja vitu vilivyotolewa kwa bibi huyo kuwa ni pamoja na mchele, mahindi, unga, sabuni, sukari, jiko la gesi, godoro na fedha kiasi cha zaidi ya Sh.milioni mbili iliyowekwa katika mfuko maalum wa M-Koba ambao utatumika inapokuwa na uhitaji wa kitu.

"Sisi tumeguswa na kuchangia kile kilichopo ndani ya uwezo wetu ili kuhakikisha familia hii inapata mahitaji muhimu ya watoto, tunawaomba wengine waguswe na kuendelea kuisaida familia mpaka watoto wakue," alisema Bundala.

Ofisa Maendeleo wa Kata hiyo, Catherine Phaeles, alivishukuru vyombo vya habari kwa kuchapisha habari za tukio la watoto hao kutelekezwa na kusababisha wasamaria wema kujitokeza na kumsaidia bibi huyo.

Catherine, alisema wamefungua akaunti benki kwa ajili ya kukusanya fedha zinazochangwa na wasamaria badala ya simu ya mkononi kwa sababu usalama wake ni mdogo na kumuepusha kutapeliwa na matapeli.



Mkuu wa Wilaya ya Musoma, mkoani Mara, Juma Chikoka akiwa na sururu yake alipokuwa akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Kigera Etuma, kabla ya kushiriki kazi ya kuchimba msingi, kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Sekondari Kigera Mwiyale, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafanyabiashara: Serikali itoze kodi kwenye faida

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAFANYABIASHARA mkoani hapa wameiomba serikali kuondoa kodi ya ushuru wa huduma na kutoza kwenye faida badala ya mtaji.

Walitoa ombi hilo juzi wakati wakitoa mapendekezo kwenye mkutano wa Tume ya Rais ya Uboreshaji wa Kodi.

Mfanyabiashara wa kituo cha mafuta, Mayengo Bageni kutoka wilayani Kahama, alisema tatizo la utozwaji wa kodi hiyo ni kubwa na linawadidimiza kiuchumi wafanyabiashara kutokana na kutozwa kwenye mtaji na siyo sehemu ya faida kama kodi zingine.

Alisema tatizo lingine ni taasisi mbili kutoza kodi ya aina moja, akitolea mfano ya mabango barabarani ya kutangaza biashara zao.

Alisema katika mabango hayo, halmashauri inatoza kodi na Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) nao wanatoza kodi bango hilo hilo.

Katibu wa Chama cha Wachimbaji Wadogo wa Madini Mkoa wa Shinyanga (SHIREMA), Gregory Kibusi, alipendekeza kuondolewa kwa utiriri wa kodi kwa wachimbaji hao ili walipe kihalali na wao wapate faida.

Mwakilishi wa Wakulima Wadogo, Kulwa Dotto, alishauri kuondolewa kwa tozo kwenye mazao kutoka shambani na kupelekwa nyumbani kwa kuwa hawaendi kufanya biashara bali ni kuyahifadhi.

Kaimu Mratibu wa Shirikisho la Wafanyakazi nchini (TUCTA) Mkoa wa Shinyanga, Laurean Kyombo, alishauri kuondolewa kwa kodi kwenye malipo ya posho kwa watumishi wa sekta binafsi kama ilivyo kwa watumishi wa serikali.

Kyombo, aliiomba serikali kuondoa kodi kwenye zawadi za wafanyakazi bora Siku Wafanyakazi Duniani, Mei Mosi na kutokatwa kodi kwenye mafao ya wastaafu.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Julius Mtatiro, alisema katika taifa lolote duniani, ulipaji kodi ni chanzo kikubwa cha mapato cha kuliwezesha kutekeleza miradi ya maendeleo.

Kaimu Mwenyekiti wa Tume hiyo, Leonard Mususa, alisema imeundwa baada ya kuwepo kwa malalamiko mengi juu ya utitiri wa kodi na tozo.

Mususa, alisema kwa sasa ulipaji wa kodi nchini upo chini ikilinganishwa na Nchi za Kusini mwa Jangwa la Afrika Sahara.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan anataka kupata mapendekezo ya uboreshaji wa mifumo ya kodi na kupunguza malalamiko ili kila mmoja atimize wajibu wake ipasavyo.

## CHADEMA Butimba wataka kiongozi mwajibikaji

**Na Remmy Moka,** MWANZA

WAKATI Wajumbe wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wakianza mchakato wa kupiga kura kuchagua Mwenyekiti na Makamu Taifa, wanachama wa chama hicho Kata ya Butimba jijini Mwanza wamewataka kumchangua kiongozi muwajibikaji.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti katika mdahalo, wanachama hao akiwemo Antherius Audax, Katibu wa Chadema Kata hiyo, alisema wajumbe wanatakiwa kuchagua kiongozi atakayekuwa na uwezo wa kusimamia utekelezaji wa matakwa ya kikatiba.

Audax, alisema miongoni mwa vitu ambavyo havifuatwi katika katiba ni mgawanyo wa fedha za chama kwa gazi za chini ili kusaidia kuendesha shughuli zake.

Alisema binafsi anamuunga mkono Tundu Lissu kuwa mgombea wa uenyekiti wa chama hicho na kuwa ana imani juu ya malengo yake ya kuongoza kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za katiba.

Mwenyekiti mstaafu wa CHADEMA wa Kata hiyo, Petro Kassa alisema kwa sasa chama hicho bado kinamuhitaji Freeman Mbowe hasa kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu ili kupata viti vya kutosha vya wabunge na madiwani.

"Sera ni zilezile za chama ninachojua hata akiletwa Lissu lazima atekeleze matakwa ya chama, mimi bado ninaona Mbowe anafaa," alisema Kassa.

John Kimori, alisema ana imani na Lissu kuwa ndiye atakaye wavusha katika kila hatua hasa kuelekea kwenye uchaguzi huo wa mwaka huu utakaovishirikisha vyama vingi vya siasa.

"Uongozi unaitaji mtu mthubutu wa masuala yaletayo maendeleo katika kila nyanja zote ambaye ni mkweli, muadilifu na mpenda haki ambaye akiona viashiria vya upotevu wa haki anakuwa mstari wa mbele kuvikemea," alisema Kimori.

Elias Inyonga, alisema Lissu ana uwezo wa kukiongoza chama hicho kwani ni moja ya kiongozi mpinga rushwa na muwajibikaji kwa chama na amekuwa akikemea kila aina ya viashiria vya vitendo hivyo ndani na nje ya chama hicho.

Mwenezi wa CHADEMA wa Kata hiyo, Kapama Sambali, alisema anamuunga mkono Lissu kwa sababu siyo mgombea kigeugeu na mifumo ya kiutendaji ndani ya chama hicho, anayo misingi thabiti, mtu asiyeyumbishwa na maneno yasiyo na tija.

Mwenyekiti wa Chama hicho Tawi la Kanyerenyere, Vitaris Reonidas, alisema anamuunga mkono Lissu kwasababu anahitaji wajumbe wa mkutano mkuu kutokubali kukiua chama kwa kukubali kurubuniwa na wagombea kupitia rushwa.



Ukurasa 12

**Uhaba wa maji ulivyo chanzo cha misukosuko ya kijinsia**



Ukurasa 13

Vipodozi havijaguswa lakini ni adui wa afya na mazingira



Ukurasa 14

**Bila ulinzi mazingira, ikolojia bwawa la JNHPP litatetereka**

Nipashe
TESA
Jumanne Januari 21, 2025
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

ELIMU

NA MAULID MMBAGA

DIRA 2050

# Wadau wahimiza ulazima kuinua elimu, sayansi na teknolojia

• Maslahi manono walimu ni lazima

ULAZIMA wa Tanzania kufanya mapinduzi ya elimu, sayansi na teknolojia ni hoja zinazotawala maoni ya makundi mbalimbali yanayosikika wakati wa kuhakiki rasimu ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050.

Wadau wanataka iwepo mikakati madhubuti ya kusongesha mbele sekta hizo ili kufikia mabadiliko na maendeleo endelevu ifikapo mwaka 2050.

Ni katika mkutano baina ya Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji na makundi mbalimbali wakiwamo viongozi wa dini, wafanyabiashara, wazee, vijana, wanasiasa, wenye ulemavu, wadau wa maendeleo, mabalozi na mashirika ya kimataifa, katika mchakato wa kukusanya maoni yatakayojumuishwa katika kuandaa dira hiyo.

Kwenye vikao vilivyofanyika kwa nyakati tofauti wajumbe wanasisitiza kuboresha mifumo ya kutoa elimu pamoja na kufanya jitihada za makusudi za kuwafanya Watanzania kuwa na uelewa wa kutosha wa matumizi ya teknolojia katika shughuli mbalimbali.

Mfanyabiashara Judith Mhina, akatia maoni yake , anashauri kwamba ni muhimu mwalimu kulipwa kiasi cha kutosha , pamoja na kuhakikishiwa maisha bora na kuwa na kipato cha kumudu gharama za maisha ili wawaandae vyema wanafunzi.

Judith anaishauri serikali kutathmini upya mishahara ya watumishi wa umma wakiwamo waalimu ili kuendana na mabadiliko ya gharama za maisha, akieleza kuwa ili kuwa na jamii bora ni muhimu waalimu wawezeshwe kikamilifu na kuishi maisha ya kufanana na hadhi zao.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, akizungumzia mikakati ya kuboresha sekta za elimu, sayansi na teknolojia. **PICHA: MAULID MMBAGA**

Anashauri serikali kuanza kuweka kipaumbele katika mafunzo na malezi ya watoto, kuanzishwe utaratibu wa kujifunza kuhusu teknolojia ya akili mnemba (AI), pamoja na kufundishwa kujitegemea na kujilinda dhidi ya mashambulizi mbalimbali ya kimwili kwenye mitandao ya kijamii na kule wanakoishi.

Naibu Katibu Mkuu wa Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Shekhe Mohamed Khamis, anashauri kuboresha maslahi ya walimu ili kuwaongezea motisha na nguvu za kiuchumi, akieleza kuwa itajenga jamii iliyoelimika kuelekea miaka 25 ijayo.

Pia anahimiza umuhimu wa serikali kusimamia ratiba na mapumziko kwa wanafunzi wa shule za serikali na binafsi ili kuwa na ulinganifu wa masomo na mapumziko kwa wanafunzi, ili washiriki shughuli zingine.

Mkuu wa Programu za Umoja wa Mataifa Tanzania (UNA-Tanzania) Lucas Kifyasi, anasema suala la elimu halijawekwa kama moja ya sekta za kimageuzi wakati dira 2050 itatakiwa kutekelezwa katika kipindi cha mapinduzi ya nne ya viwanda ambayo teknolojia itahitajika zaidi.

Anashauri kuwa dhana ya teknolojia inaendelea kukua, hivyo ni muhimu kuheshimu elimu ambayo ndiyo nyenzo kuu katika kuhakikisha kwamba teknolojia inarithishwa vizazi na vizazi, huku akisisitiza elimu iwekwe kama sekta ya kimageuzi kwenye dira 2050.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni za GSM, Benson Mahenya, anashauri kwamba kuna haja ya kufundisha elimu ya biashara kuanzia chekechea hadi vyuoni ili vijana wakue na kuelewa kuhusiana na masuala ya kibiashara.

**TEKNOLOJIA**

Mkurugenzi wa Programu za Maendeleo na Utetezi wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Azgard Stephen, anasema ni muhimu pia kutolewa kipaumbele katika masuala ya sayansi, teknolojia, na diplomasia katika mapinduzi ya kiuchumi na kijamii.

“Sisi CCT tuliangalia suala la sayansi na teknolojia kwa kuzingatia jinsi dunia ilivyobadilika na mapinduzi yanayotokea. Tunapendekeza diplomasia iwe sehemu ya vichocheo vya maendeleo ili kuwezesha Tanzania kujihusisha vyema katika biashara za kimataifa na kujitengenezea nafasi bora kikanda na kimataifa,” anasema Azgard.

Stephen anaongeza kuwa mapinduzi ya kidijitali ni mojawapo ya vichocheo muhimu vya maendeleo vilivyotajwa katika rasimu ya dira hiyo, akibainisha umuhimu wa kuendelea kuwekeza katika teknolojia na sayansi ili kufanikisha malengo ya taifa.

“Mpango wetu umetaja umuhimu wa sayansi na teknolojia kama kichocheo cha maendeleo. Tunashauri diplomasia nayo izingatiwe kama kichocheo, hasa katika nguzo ya uchumi ambayo inazungumzia ushiriki wa Tanzania katika jumuiya za kikanda na kimataifa,” anasema.

Mtaalam wa Programu wa Takwimu za Kijinsia kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Wanawake (UN Women) , Dk. Sadananda Mitra, anasema kiwango cha uelewa wa kusoma na kuandika kwa Watanzania ni kizuri, lakini hawapaswi kuishia hapo.

“Lazima tuangazie vipengele kama muunganisho wa intaneti na matumizi ya teknolojia ya akili mnemba hasa vijijini. Hii itawahakikishia watu wa maeneo hayo ushiriki kikamilifu katika mchakato wa maendeleo,” anasema Dk. Mitra.

INAENDELEA UK.13

ELIMU

NA JULIETH MKIRERI

# Uhaba wa maji ulivyo chanzo cha misukosuko ya kijinsia

• Hofu wengine kuvunjika ndoa, kuacha watoto wenyewe usiku

“HALI ilikuwa ngumu kwenye familia zetu muda mwingi ni kuwaza nitapata maji leo? Kukaa kisimani kusubiri maji wakati mwingine kulazimika kukesha kuyangoja yakusanyike huku tukiwaacha watoto pengine wagonjwa peke yao usiku nyumbani.”

“Upo muda unapata changamoto za akili na hata kuchanganyikiwa kwa kukosa maji nyumbani. Hakuna ya kupikia, kufulia wala kunywa lakini pia kuwaacha watoto peke yao nyumbani na kutembea usiku na hata wa manane ni adha,” anasema Saida Munishi.

Ni mkazi wa Kitongoji cha Mjembe kata ya Kibindu, mkoani Pwani, akitaja machungu yanayoumiza kinamama wakati wa kusaka maji anapozungumza na Nipashe.

Anaongeza kuwa ni mengi hasa umbali na kisima walichokuwa wakitumia wakikosa maji ya uhakika au kuwa vigumu wengi kuyapata.

Ni jambo lililosababisha kutumia muda mwingi kusaka huduma hiyo, kuwaza na kuwazua lakini pia kuongeza hofu kwa wanafamilia wengine wanaobaki nyumbani hasa watoto na wenye mahitaji wakiwamo wagonjwa.

“Kuna wakati wanaume pia wanakuwa na wasiwasi tunapochelewa kisimani lakini ilifikia kipindi wakaanza kuwasindikiza wake zao. Ni hasa wanapokosa maji mchana inawalazimu kwenda kukesha kisimani kusubiri maji na tunarejea nyumbani usiku mnene,” anasimulia.

Anasema hali hiyo inathibitisha ukweli kuwa ukosefu wa huduma muhimu za kijamii hasa maji, tiba na nishati vinarudisha nyuma maendeleo ya wanawake na kuongeza pengo la ukosefu wa usawa kijinsia, kijamii na kiuchumi.

Anasema pia kunasababisha baadhi ya shughuli zao kwenda kinyume na mipango huku wakiwa chanzo cha watoto kuchelewa kula, kusoma, kuwa na mazingira masafi kisa kukosekana maji.

Saida anaishukuru serikali kwa kuwachimbia bwawa la maji linalowawezesha kupata maji karibu na maeneo yao na pia kufanya vizuri shughuli zake za mama lishe ambazo awali alikuwa akifanya kwa kusuasua kutokana na shida ya maji.



Baadhi ya wakazi wa kitongoji cha Mjembe wakifua karibu na bwawa kabla ya RUWASA kuwafikishia maji ya kisima. **PICHA: JULIETH MKIRERI**

> Kuna wakati wanaume pia wanakuwa na wasiwasi tunapochelewa kisimani lakini ilifikia kipindi wakaanza kuwasindikiza wake zao.

“Lakini pamoja na shukrani tunachoomba sasa ni Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) watuunganishie maji yafike karibu na makazi yetu. Vituo vya maji vikiwa maeneo ya nyumbani shughuli nyingi za maendeleo zitafanyika,” anasema.

Anaeleza kuwa kwa sasa watoto wao wanaishi kwenye mazingira safi tofauti na ilivyokuwa kabla ya kuwepo kwa bwawa hilo ambapo maji ya kufulia yalipatikana kwa nadra.

Fatuma Ramadhani mkazi wa Mjembe, anasema eneo ambalo walikuwa wakifuata maji kabla ya kuwapo bwawa hilo walitembea zaidi ya saa moja tofauti na sasa ambapo maji yanapatikana karibu na yanawawezesha kufanya shughuli zao za nyumbani na kiuchumi kwa wakati.

Bwawa hilo ambalo ni chanzo cha kisima kitakachojengwa Mjembe unakwenda sambamba na ujenzi wa kisima hicho ambacho ni kati ya 40 vinavyojengwa mkoani Pwani.

Mbali ya Mjembe katika kata ya Kibindu pia wakazi wa Kitongoji cha Diagala Kijiji cha Dihozile wamefikishiwa huduma ya maji ya kisima na kuondokana na kutumia maji ya malambo.

Mmoja wa wakazi wa Diagala, Lucy Kilekeni anaishukuru serikali kwa kuwafikishia huduma hiyo na kuwaondolea adha ya kununua dumu la lita 20 kwa Sh 1,000.

Lucy anasema kabla ya mradi huo kufika katika kitongoji chao walikuwa wanalazimika kutumia maji ya lambo na kununua ya kunywa yaliyokuwa yakipatikana mbali

Meneja wa RUWASA, Beatrice Kasimbazi anasema visima hivyo vinachimbwa kupitia mradi wa uchimbaji wa visima.

Anasema visima 40 vitakavyochimbwa kwa mkoa wa Pwani vipo katika mradi wa visima 900 vitakavyochimbwa katika mikoa mbalimbali kusogeza huduma ya maji karibu na wananchi.

Aidha, kupitia mradi huo wa visima wakazi 32,750 katika mkoa huo wanatarajia kunufaika na kwamba vingi vitachimbwa katika majimbo nane kati ya tisa.

Beatrice anasema Sh bilioni 2.4 zitatumika katika utekelezaji wa programu hiyo inayofanyika na kwamba utekelezaji wa mradi huo wa visima kwa mkoa wa Pwani ulianza Agosti 2024.

Meneja huyo anasema mbali ya mradi wa visima pia ipo miradi 35 yenye gharama ya bilioni 35.8 ambazo inaendelea kutekelezwa.

Anasema ikikamilika itahudumia wakazi 180,528 na kuongeza hali ya upatikanaji wa maji kwa asilimia 8.1 na hivyo kufanya mkoa kuwa na asilimia 88.4 ya upatikanaji wa maji ifikapo Desemba mwaka huu.

Mhandisi anasema katika mradi wa visima maeneo yaliyopewa kipaumbele ni yale ambayo hayakuwa na huduma ya maji kabisa hicho ndio kilikuwa kigezo kikubwa.

“Kati ya visima hivi 40 vinavyojengwa Pwani itapata visima virefu 35 . Vinachimbwa na vitano vinatumia vyanzo mbadala ikiwamo mabwawa na ifikapo Januari 30 vyote vitakuwa vimekamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi,” anasema .

Halikadhalika anasema ushirikishwaji wa wananchi na elimu vinaendelea kufanyika kuhakikisha miradi hiyo inalindwa kwa ajili ya kuzuia uharibifu wa vyanzo vya maji na miundombinu ya maji.

Hivi karibuni Naibu Waziri wa Maji, Kundo Matthew anafanya ziara katika mkoa wa Pwani akikagua miradi ya visima inayosimamiwa na RUWASA pamoja na mingine ya DAWASA.

Akiwa katika ziara hiyo anasema ajenda ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuwapatia maji safi na salama wananchi karibu na makazi yao jambo ambalo kwa mkoa huo linatekelezeka kwa kasi.

Katika ziara hiyo anazungumza na wananchi ambao aliwakumbusha kutunza miundombinu ya maji ili huduma hiyo iwe endelevu.

“Wananchi tunzeni miundombinu ya maji ili adha mliyokuwa mnaipata isijirudie, serikali imewekeza fedha nyingi kwenye miradi ya maji ili shughuli zenu zisikwamishwe na kukosa huduma hii, ni mpango wa Raisi wetu wa kumtua mama ndoo kichwani tunautekeleza kwa vitendo,” anasisitiza.

Miradi ya maji inayojengwa kwa mkoa huo gharama ya kununua maji ndoo moja kutoka kwenye vituo haizidi Sh. 100 kulingana na utaratibu uliowekwa na wananchi na yapo maeneo makundi maalumu wakiwamo wazee hupata huduma hiyo bure.

ELIMU
NA GAUDENSIA MNGUMI

# Vipodozi havijaguswa lakini ni adui wa afya na mazingira

• Vifungashio vya plastiki, nywele bandia

KUJIPODOA kwa wanawake na wanaume hasa mijini na vijijini kwa kiwango kinachoongezeka kila mara ni jambo ambalo hivi sasa linazidisha changamoto kwenye mazingira na afya za watumiaji.

Hatari si kwenye kutumia vipodozi vyenye viambato vya sumu pekee lakini pia kuchafua mazingira na kutishia hatima ya viumbe majini na ardhini.

Vipodozi hutumiwa na mabilioni ya watu kuanzia wanasiasa, watu maarufu na mashuhuri duniani, wanapaka kucha rangi, dawa kwenye nywele za asilia ,mafuta na krimu kwenye ngozi, urembo maalumu usoni, kwenye meno, manukato, rangi za midomoni na nywele bandia rasta kuvaa wigi.

Japo hakuna takwimu lakini huenda tasnia ya vipodozi ndiyo inayokua kwa kasi kuliko nyingine muhimu mijini na vijijini ikihusisha wafanyabiashara wakubwa wa nje na ndani ya nchi. Ushuhuda uliopo kwenye majiji na miji kama Dodoma, Mwanza, Mbeya, Moshi, Iringa na Dar es Salaam unaonesha kwamba karibu kila kona kuna duka la vipodozi na saluni za kike na kiume.

Kadhalika stendi au vituo vingi vya mabasi vimesheheni vibanda vya vipodozi kuanzia krimu za kuchubua na kung'arisha sura, manukato au marashi, mafuta ya ngozi, nywele na rangi za aina mbalimbali kubadilisha nywele, ndevu na pia dawa za kuweka kwenye nywele hasa 'relaksa na wevu.'

Wanapatikana pia wanaoosha na kupaka kucha rangi na zama hizi wameongezeka zaidi.

Wauza urembo kwenye pikipiki na baiskeli ni wengi mno, yote yakiashiria kuwa hiyo tasnia ni kubwa na muhimu.



Shehena za vipodozi zinazoingizwa nchini kila mwaka haziyaachi mazingira salama. **PICHA: MTANDAO**

Ni wakati sasa mamlaka za miji, majiji na vijiji zikafanya sensa ili kujua idadi au kuna maduka mangapi ya vipodozi na saluni za wanawake na vinyozi maeneo yao maana ni sekta inayokua kwa kasi na kuilazimisha kuchukua thadhari za kulinda mazingira na afya za wateja.

Mara nyingi wananchi wamesikia kutoka Shirika la Viwango (TBS) kuhusu kuwapo vipodozi vyenye viambato vya sumu, lakini ni vyema waende mbali na kuwaeleza wananchi kuhusu kiwango cha vipodozi vinavyoingizwa nchini na athari zake kimazingira.

Kadhalika, Mamlaka ya Mapato (TRA), halmashauri za miji, majijini na vijiji zisaidie kwa kubainisha idadi ya leseni za biashara zinazotolewa kila mwaka kwa ajili ya kuuza vipodozi na fedha zinazokadiriwa kupatikana na idadi yawatu waliojiajiri huko.

Mambo yasiishe hapo Wizara ya Fedha ione namna ya kuongeza kodi ya vipodozi katika bajeti yake ya 2025/ 26 kwa sababu sekta ya urembo inakua kwa kasi na 'inalipa' kwa lugha ya mijini.

### HATARI ILIYOPO

Licha ya kutoa nafasi za ajira kwa maelfu ya vijana na kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa mataifa Afrika yenye wasichana walimbwende na wanaume watanashati uhifadhi wa mazingira uko hatarini.

Ni kutokana na vifungashio vya vipodozi na mamilioni ya tani za nywele bandia zinazotumiwa mkwenye ulimbwende.

Sekta ya vipodozi inastahili lawama kwani ni chanzo cha kukwamisha mikakati ya kukabiliana na uchafu wa mazingira hasa kujaza vifungashio kama makopo na mikebe ya plastiki kila mahali.

Tani za mamilioni ya mikebe ya kubebea urembo kuanzia krimu, poda, mafuta na vimiminika hutupwa kila mahali lakini mwisho zinaishia baharini au kwenye maziwa baada ya kujazwa kwenye mito na mikondo ya maji.

Athari za moja kwa moja ni vifo vya samaki na viumbe wengine wanaoishi majini na pia binadamu wanadhurika hasa kutokana na viambato vya sumu kutoka kwenye bidhaa feki za urembo.

Urembo kama nywele bandia au rasta na wigi zinatumiwa na mamilioni ya wanawake. Zinatumika mara moja na kutupwa hivyo kuongeza taka nyuzi za plastiki kila mahali.

Zimejaa ardhini, baharini na angani kwa vile zipo zinazochomwa na moshi wake mara moja unachufua anga.

Mabilioni ya tani za vipodozi hutengenezwa kila mwaka duniani na kuingizwa Tanzania pia na mikebe, mifuko ya nailoni, chupa na makasha yake hutupwa kila mahali kuanzia kwenye mashimo ya taka, kufukiwa ardhini, zikitoka kwenye saluni za kike na kiume, nyumbani, shuleni na popote penye watu.

Cha kusikitisha ni kwamba vifungashio hivyo vya plastiki na nywele bandia kwa kiwango kikubwa zaidi ya asilimia 70 huingia kwenye vyanzo vya maji kama maziwa na mito na mwisho hujaa baharini.

Ndiyo maana Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP) linatabiri kuwa endapo mifuko, , vyombo na vifungashio vya plastiki havitapigwa marufuku kufikia 2050, bahari na maziwa yatajaa plastiki kuliko samaki.

Aidha, UNEP mwaka 2015 ilitoa ripoti kuwa baadhi ya vipodozi vimesheheni chembechembe za plastiki ambazo ni hatari kwa mazingira. Chembechembe za plastiki zinaonekana kwenye rangi za kucha, inasema UNEP.

UNEP inasema chembechembe za plastiki kwenye vipodozi zinajaa baharini au ndani ya vyanzo vya maji na ardhini kwa miaka mingi vikitishia ikolojia.

Pamoja na TBS kukamata vipodozi feki kila mwaka ikumbukwe kuwa bidhaa hizo ni hatari kwa afya ya wateja na kwa mazingira na sasa taifa lianze kampeni za kuamua jinsi ya kudhibiti vifungashio vya vipodozi.

Aidha, na nywele bandia nazo zisisahaulike kwa maana kila dakika zina wateja wanaofumua, kutupa na kusuka nyingine, kadhalika mawigi nayo yakitupwa au kununuliwa mapya, vyote vikiongeza taka za nyuzi za plastiki majini na ardhini. Hivyo usimamizi ni lazima maana vinaongeza uchafuzi wa mazingira.

## Wadau wahimiza ulazima kuinua elimu, sayansi na teknolojia

**INATOKA UK.11**

Anasisitiza umuhimu wa sera zinazoongozwa na ushahidi, akieleza kuwa upungufu wa data au upatikanaji wa data usio kamili umekuwa changamoto katika nyaraka nyingi za sera zilizopita, akishauri teknolojia kuhusishwa zaidi ili kuongeza ufanisi.

"Tunapaswa kuimarisha mifumo ya kukusanya data na kutumia takwimu sahihi na zilizogawanywa vizuri kufuatilia maendeleo yetu," anasema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Hanspaul, Satbir Hanspaul, anasisitiza kuwa kwenye elimu kuna umuhimu wa kuwa na mitaala yenye kujumuisha masomo ya uchumi na biashara kwa kiasi kikubwa kwani Watanzania wengi wamekuwa na changamoto ya kushughulika na masuala ya fedha jambo ambalo kwa mtazamo wake anaona linalirudisha nyuma taifa.

Anasema matumizi ya mifumo ya kidijitali na AI yameongezeka maradufu miongoni mwa kampuni, benki na wafanyabiashara hata ambao wapo mbali na miji kitu ambacho hakikuwepo kwa miaka 25 iliyopita.

"Kwenye rasimu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 sijaona jambo hili likiangaliwa sana, kwamba sisi Watanzania tunatumiaje fursa ya AI ?" anahoji Hanspaul.

MALENGO

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo anasema suala la elimu tangu mwaka 2000 serikali ilijiwekea lengo kwamba ifikapo 2025 angalau asilimia 90 ya watoto wanaomaliza shule za msingi waende sekondari, wakati huo ikiwa chini ya asilimia 20.

Anaeleza kuwa ilipofika 2022 walifanya tathmini walibaini kwamba takribani asilimia 70 ya vijana wanaomaliza shule za msingi wanakwenda sekondari na kwamba tathmini ya mwaka jana ilionesha ni asilimia 78. "Tunaamini hadi mwisho wa mwaka huu tutakuwa tumepiga hatua zaidi".

ELIMU

NA DK. FELICIAN B. KILAHAMA

# Bila ulinzi mazingira, ikolojia bwawa la JNHPP litatetereka

BWAWA la kufua umeme la Mwalimu Nyerere (JNHPP) zamani Stigler's Gorge, ndani ya Mto Rufiji tangu mwanzo ni kazi iliyokuwa itekelezwe kati ya 1975 na 1985.

Itakumbukwa ni wakati wa awamu ya Mwalimu Julius Nyerere, lakini matarajio yalififia taifa lilipoingia kwenye vita vya Uganda kati ya miaka 1978 na 1980.

Baada ya vita na nchi kujihakikishia usalama rasilimali nyingi zilitumika kuwaondoa wavamizi, Tanzania ikajikuta kwenye changamoto lukuki kiuchumi.

Kutokana na hali hiyo mradi wa bwawa la Stigler's Gorge au sasa JNHPP kwa kutumia maporomoko ya Mto Rufiji, likawekwa kiporo. Ili kukidhi mahitaji makubwa ya umeme wa gharama nafuu kuliko unaotokana na mafuta, serikali ilijenga mabwawa ya Kidatu mkoani Morogoro na Mtera mpakani mwa Iringa na Dodoma kufua umeme wa maji ya Mto Ruaha-Mkuu.

Vilevile, iliendelea kutumia umeme wa bwawa la Nyumba ya Mungu mkoani Kilimanjaro na jingine eneo la Hale la Pangani, mkoani Tanga yaliyokuwa yamejengwa kabla ya uhuru 1961 na TANESCO ikiendelea kuyapanua baada ya uhuru na leo yanachangia umeme kwenye gridi ya taifa.

Pamoja na juhudi hizo, bado kuna dosari za upatikanaji umeme wa uhakika.

Upo usemi kuwa 'hayawi hayawi huwa' ikimaanisha kilichoshindikana awali sasa kinawezekana kama ilivyokuwa mradi wa mkakati kujenga bwawa kubwa kutumia maji Mto Rufiji ili taifa liwe na umeme kamilifu.

Naipongeza serikali awamu ya tano ambayo Rais Samia Suluhu Hassan wa awamu ya sita, alikuwa Makamu wa Rais wakati juhudi za kuanza utekelezaji mradi zilipoanza.

Kama siyo uthubutu, umakini wa aliyekuwa Rais wakati huo, John Magufuli, alipodhamiria kujenga JNHPP huenda leo shida ya umeme ingekuwa kubwa.

Kama siyo uthubutu huo, sipati picha hali ingekuwaje kuhusu kuwapo nishati hiyo ya uhakika nchini. Kadhalika, serikali ya awamu ya tano imekuwa chimbuko la miradi ya kimkakati kadhaa ambayo awamu ya sita inaimaliza na kusongambele.

Pia, inatekeleza miradi mingine kadri inavyoona inafaa. Kupitia juhudi hizo wengi sasa wana ufahamu wa kutosha kuwa tukidhamiria kwa dhati na kukawepo nidhamu,maadili kwa viongozi hakika Afrika inaweza kujikwamua kiuchumi bila kutegema sana misaada kutoka nje.



Maji yakiwa yamejaa kwa kiwango kinachozalisha megawati 1, 400 za umeme katika bwawa la JNHPP. **PICHA: MTANDAO**

JNHPP inalenga kulipatia taifa megawati zaidi ya 2,100 sasa upo ukingoni, ni jambo la kujivunia. Taarifa kutoka TANESCO kwenye vyombo vya habari zinaeleza kuwa bwawa limefikia hatua ya mitambo ya kufua umeme kuwashwa na kutoa megawati 1,410 karibu asilia 70 ya kiwango cha megawati zinazotarajiwa.

Kadhalika, imethibitishwa kuwa njia za kusafirisha umeme kutoka Mto Rufiji hadi Chalinze zimekamilika kwa asilimia 99. Aidha, kituo cha kupoza umeme kinachojengwa Chalinze kimekamilika kwa asilimia zaidi ya 97 yakiwa ni mafanikio makubwa.

Mafanikio na miradi mingine ya kufua umeme na megawati kwenye mabano ni Rusumo (80) na Kinyerezi 1 (185) yameipa nguvu serikali ambayo kupitia wakala wa kusambaza umeme vijijini (REA), mwisho wa mwaka 2024 imesambaza umeme kwenye vijiji zaidi ya 12,000.

Vilevile, kufika mwisho wa 2024 vitongoji zaidi ya 32,000 vimefikishiwa umeme kati ya vitongoji 64,359. Kwa takwimu hizi tunajivunia uwepo wa JNHPP kama kiini cha kuchochea maendeleo nchini pamoja na mataifa mengine yatakayonunua nishati hiyo.

Kuwepo bwawa la JNHPP ni suala moja lakini kuwepo matumizi endelevu bila kuathirika mifumo ufuaji umeme ni jambo jingine.

### UHAI JNHPP

Hoja ya msingi ni kuhusu bwawa JNHPP kubaki katika uzima na kuzalisha umeme kwa miaka mingi ijayo.

Maji ya mto Rufiji yanatokana na vyanzo vya mito na vijito kutoka mikoa mingine nje ya mkoa wa Pwani bwawa lilipo yanahitaji kulindwa.

Mto huo ni muunganiko wa maji ya mito Ruaha Mkuu, Kilombero na Kihansi na kwamba Ruaha Mkuu vyanzo vyake vikuu ni vijito mbalimbali katika mikoa ya Iringa na Mbeya ikiwemo pia Mto Ruaha Mdogo wenye vyanzo vyake katika wilaya ya Mufindi hapa kuna eneo muhimu la shamba la miti la Saohill.

Mito Kilombero na Kihansi hupata maji kutoka sehemu mbalimbali mkoani Morogoro.

Ukifuatilia mito na vijito hutoka mlimani, kuelekea ziliko shughuli za binadamu; unakuta maji yamesheni taka, udongo, tope, mchanga na takangumu.

Mito mingi nchini vyanzo vyake ni kwenye maeneo kadhaa yenye shughuli kemkemu za mfano, Ruaha Mkuu unatokea juu milimani na kuteremkia wilayani Mbarali kuelekea kwenye ukanda wa wakulima ya mpunga ikiwamo mashirika makubwa na wakulima wadogo ambao tegemeo kubwa ni maji ya Ruaha Mkuu.

Mto unapoelekea Hifadhi ya Taifa Ruaha, unapita eneo oevu la Ihefu ambayo ni sehemu ya kuhifadhi maji yanayoendelea kutiririka Ruaha Mkuu.

Eneo hilo muhimu mara kwa mara hughubikwa na changamoto za kuingiza makundi makubwa ya mifugo nyakati za ukame na kusababisha madhara makubwa kwenye ikolojia na uoto asili unaofanya maji yatuame au kuhifadhiwa muda mrefu.

Matokeo hasi husababisha maji kwenye Ruaha Mkuu kuwa hafifu na kupelekea mahangaiko makubwa kwa wanyamapori katika Hifadhi ya Taifa Ruaha pia kuathiri kufua umeme kwa kiasi kikubwa.

### KULINDA JNHPP

Kama kweli tumedhamiria kuhakikisha JNHPP inastawi kwa miaka mingi, na kutokana na ukweli kuwa mito inayopeleka maji hadi mto Rufiji, imo kwenye sehemu zenye shughuli nyingi za binadamu zisizoendelevu hasa kilimo na ufugaji ni dhahiri hatua kali lazima zichukuliwe kuhakikisha maji yanaendelea kutiririka katika mito hiyo.

Ni lazima yalindwe yawe safi kwa kuzingatia yafuatayo : Mosi ni usimamizi, utekelezaji endelevu wa sera, sheria na kanuni za kulinda na kutunza mazingira zikiwemo sheria za mazingira, misitu na nyuki na nyingine za kisekta na kuimarishwa kwa ngazi zote za uongozi,utawala nchini.

Uzoefu unaonyesha kuwa sera, sheria, kanuni na miongozo vipo isipokuwa utekelezaji ni changamoto ainayake.

Tunahitaji nidhamu na kudhamiria na usimamizi makini kwa ajili ya kuimarisha uwezo wa mifumo ikolojia ya kuchuja maji ya mvua yaweze kuingia kwenye mito ili udongo na tope pamoja na taka nyinginezo vibaki juu ya ardhi.

Pili, kulima, makazi na mifugo kandokando ya mito na vijito tangu mwanzo hadi mwisho baharini au kwenye maziwa na mabwawa, zidhibitiwe bila kuoneana haya ili kulinda mifumo ikolojia.

Kifungu 57 (1) cha sheria ya usimamizi wa mazingira (2004), kinazuia shughuli za binadamu ambazo kwa asili yake, zinahatarisha sana 'uhai' wa eneo la hifadhi ya mita 60 linalotakiwa kulinda mazingira yasiharibike husasani ni ardhioevu ikiwamo bahari, mito, mabwawa na maziwa;

La tatu tuhakikishe wakati wote ukanda wa mita zilizoainishwa kwenye mwongozo uliotolewa Disemba mosi, 2020 na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, unatekelezwa ipasavyo.

Kupitia waraka huo shughuli za kibinadamu zisizotakiwa kufanyika ili kulinda mifumo ikolojia kwa nia njema ya kuiweka salama na kuhakikisha mito muhimu inayoingiza maji JNHPP na mabwawa mengine, inatunzwa kwa manufaa ya wengi.

Lengo kuu likiwa ni kuhakikisha mito inatiririsha maji safi badala la kusheheni taka na tope na kusababisha vina vya mabwawa kupungua hivyo na kuathiri ufuaji umeme.

Matokeo chanya ya kuhifadhi na kulinda mifumo ikolojia ni pamoja na ukanda wa mita 60 kutoka mtoni au ziwani kuachwa na kuhakikishiwa kuwa unafunikwa na uotoasilia unaotosheleza.



**HABARI DODOMA**

# Wakulima Hombolo watakiwa kuwasilisha taarifa NIRC

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKULIMA wa Skimu ya Umwagiliaji Hombolo mkoani hapa wametakiwa kutoa taarifa sahihi kwa wataalamu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC) ili zitumike kuchangia ada ya umwagiliaji na kubaini aina ya mazao wanayolima.

Rai hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita na Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa Tume hiyo, Pascal Bilali, ikiwa ni muendelezo wa kutoa elimu kwa wakulima ya Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula nchini (TFSRP - P4R), katika skimu hiyo.

Bilali, alisema taarifa hizo ni muhimu kwa kuandaa kanzidata itakayokuwa na idadi ya skimu, vyanzo vya maji na shughuli zinazofanyika katika skimu hiyo.

Alisema takwimu hizo zitasaidia kubaini ukubwa wa shamba la mkulima, aina ya mazao na kufanya tathmini ya uzalishaji katika skimu husika.

Alisema serikali imetenga fedha kwa ajili ya kutengeneza mfumo wa kielektroniki wa usimamizi skimu za umwagiliaji nchini utakaokuwa na kanzidata ya taarifa hizo na kuzichakata kwa matumizi mbalimbali.

"Mifumo hiyo inatarajiwa kukamilika baada ya mwaka mmoja na matarajio hadi ifikapo Desemba 2025 itaanza kutumika kikamilifu hali ambayo itaongeza ufanisi katika sekta ya Umwagiliaji," alisema Bilali.

Alisisitiza kuwa ukusanyaji wa taarifa hizo utasaidia kuhifadhi takwimu za wakulima wanaoshiriki katika kilimo hicho vijana, wazee na watu wanaonufaika nacho.

"Hali hiyo itawezesha kuwa na idadi kamili ya Watanzania wanaoendesha maisha yao kupitia kilimo cha umwagiliaji, ndio maana tunasisitiza ushirikiano kwenye utoaji taarifa,"alisema Bilali.

# RUWASA yajenga miradi ya mabilioni

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MAMLAKA ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) inatarajia kutumia Shilingi bilioni 18.688 kwa ujenzi wa miradi 43 na kutoa huduma kwa watu 197,128.

Meneja wa RUWASA wa Mkoa huo, Lucas Said alitangaza mpango huo kwenye Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) kilichofanyika mwishoni mwa wiki iliyopita.

Said, alisema fedha hizo zimetengwa katika mwaka wa fedha wa 2024/2025 kwa ajili ya ujenzi wa miradi hiyo ambayo kukamilika kwake, kutaongeza upatikanaji wa huduma ya maji kwa mkoa huo kwa asilimia 12.2.

Alisema kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 5.057 ni fedha za ndani na Shilingi bilioni 13.650 ni fedha za nje.

Kwa mujibu wa Said, hadi kufikia Desemba mwaka jana mamlaka hiyo imepokea Sh.bilioni 1.489 sawa na asilimia nane kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Alisema RUWASA inaendelea kuchimba visima katika majimbo yote nane ya mkoa huo na kukamilisha visima 42 na kwamba programu hii itasaidia ongezeko la upatikanaji wa maji kufikia asilimia 85.

Akizungumza katika kikao hicho, Mkuu wa Mkoa huo, Halima Dendego, alisema pamoja na mkoa wao kuwa na maji mengi, changamoto iliyopo ni kupatikana chini ya mita 150 kwenda chini wakati uwezo wa mitambo iliyopo haifiki mita hizo.

Dendego, alisema serikali inaendelea na mwekezaji mmoja ambaye ana mitambo ya kuchimba visima vya maji mita 300 kwenda chini.

"Kama mkoa tumejiwekea lengo ifikapo Juni 2025 maeneo yote yawe na maji maana fedha zipo ila changamoto iliyopo Singida maji yapo mengi lakini yapo chini ya mita 150, " alisema.

Kwa upande wao wabunge wa mkoa huo waliitaka RUWASA kuongeza kasi ya kupeleka maji kwa wananchi ili waondokane na changamoto ya kutumia muda mwingi kusaka huduma hiyo na kushindwa kufanya shughuli za uzalishaji.



Meneja wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Singida, Mhandisi Lucas Said (kulia), akitoa taarifa ya haki ya upatikanaji wa maji wakati wa kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC), mwishoni mwa wiki. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# BMH yapigwa jeki vifaa vya maabara

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda ya Benjamini Mkapa (BMH) imepokea vifaa vya maabara ya ujuzi kwa ajili ya kufundishia afya ya uzazi kwa wanawake na upasuaji wataalam na wanafunzi wa mafunzo ya vitendo hospitalini hapo.

Vifaa hivyo vimetolewa na Klabu ya Rotary Mkoa wa Tanga na wahisani kutoka Canada kwa lengo la kuboresha huduma za afya za hospitali hiyo kwa wagonjwa kutoka sehemu mbalimbali nchini.

Akizungumza baada ya kupokea vifaa hivyo, Mkurugenzi Mtendaji wa BMH, Profesa Abel Makubi, alisema kuwa:" Tunawashukuru sana Klabu ya Rotary Tanga na washirika kutoka Canada kwa kutupatia msaada wa vifaa hivi, tutaendelea kushirikiana nao ili kuzidi kuboresha huduma zetu za afya hapa BMH."

Profesa Makubi, alisema hospitali hiyo kwa sasa imeanza mchakato wa kupandishwa hadhi na kuwa Hospitali ya Taifa.

Alisema mradi huo ni pili hospitalini hapo, ukitanguliwa na ule wa maabara ya ujuzi ambao walikabidhiwa awali na wadau hao wa sekta ya afya kuboresha huduma za afya hospitalini hapo.

Prof. Makubi aliwahakikishia wahisani hao kupitia ujumbe uliomtembelea ofisini kwake kuwa, uongozi wa BMH utaendelea kushirikiana nao na kuusimamia mradi huo kwa malengo yaliyokusudiwa.

Wakikabidhi vifaa hivyo, ujumbe huo ulielezea matarajio makubwa kuwa mradi huo wa maabara hiyo ya ujuzi utaleta manufaa kwa taifa kwa kuongezea ujuzi watalaamu wa afya kwa njia ya vitendo.

Jayesh Asher, mwakilishi kutoka klabu hiyo, alisema wana imani na huduma za kibingwa zinazotolewa hospitalini hapo.

"Tunatarajia maabara hii itatoa fursa ya mafunzo bora na ujuzi kwa wakufunzi na watoa huduma za afya walio mafunzoni," alisema.

Alisisitiza kuwa ao kama wadau wa sekta ya afya wataendelea kushirikiana na hospitali hiyo ili kuhakikisha huduma za afya zinazotolewa hospitalini hapo zinazidi kuboreshwa.





# Wakulima wahaha kusaka mbegu ya viazi mviringo

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKULIMA wa viazi mviringo mkoani hapa wameiomba serikali kuongeza upatikanaji wa mbegu za zao hilo ili kukabiliana na uhaba na kusababisha kushindwa kuzalisha kwa wingi.

Ombi hilo walilitoa mwishoni mwa wiki iliyopita kwa Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka wakati alipotembelea moja ya shamba la mkulima wa zao hilo lililopo Kijiji cha Mtwango Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

Walisema licha ya kuwa mbegu hizo zinauzwa gharama kubwa, upatikanaji wake ni mgumu kutokana na kiwango kinachozalishwa kiwandani bado hakikidhi mahitaji ya wakulima waliopo kwenye vikundi na hata mmoja mmoja.

Walisema kuna wakulima wameanza kulima zaidi ya ekari moja ya zao hilo kutokana na uhaba wa mbegu hizo kwa mwaka huu.

Mmoja wa wakulima hao, Lenard Kadali, alisema msimu wa mwaka ekari moja ya viazi alivuna gunia 136 na kuuza shilingi 65,000 kila moja.

"Changamoto kwa sisi bado inabaki ni mbegu, uhitaji wa sisi wanachama pamoja na wakulima wetu ni kulima zaidi ya hapa, ili kila mtu apate mimi nilime na yule alime inabidi 'tubalance' alisema Kadali.

Gladness Charles, alisema hiyo ni mara yake ya pili kulima viazi mviringo, msimu wake wa kwanza alipata gunia 148 kwa ekari na kuuza Shilingi 65,000 kila moja.

"Mwaka jana nililima ekari mbili, mwaka huu imebidi nilime ekari moja kutokana na changamoto ya mbegu ni chache na wakulima tupo wengi," alisema Charles.

Mwenyekiti wa Bodi ya Chama cha Ushirika Isowelo, Elia Mhonjwa, alisema chama hicho kina wanachama 630 wa zao hilo, eneo waliloomba mwaka huu ni ekari 1,279 na waliomba mbegu tani 700 na kujibiwa watapata tani 400.

Ofisa Kilimo wa Mkoa huo, Wilson Joel alisema mahitaji ya mbegu hizo mkoani humo ni tani 130,000, kati ya hizo zilizopatikana ni tani 400.

"Idadi hiyo ni zile mbegu bora, lakini wapo wakulima wanatumia hizi mbegu za shambani zinazotokana na viazi walivyolima hasa wa huko Makete," alisema Joel.

Mrajisi wa Mkoa huo, Edmund Massawe, alisema uhaba unatokana na aina ya mbegu ya Sagita kuwa na mwamko mkubwa kwa wakulima hao kwa kuwa imekuwa ikiwapatia faida kubwa wanapoitumia.

"Ukifuatilia hawa Silverland walianza na Isowelo kama mteja wake mkubwa na alikuwa amewalenga wao, lakini msimu huu wameomba tani 700 kwa sasa anapeleka mbegu maeneo mengine kama mikoa Kilimanjaro, Arusha, Iringa na Mbeya kwa hiyo yeye anaangalia kuongeza soko lake," alisema Massawe.

Akijibu ombi hilo, Mtaka alisema ipo haja ya kuhamasisha watu wengi kuja kuzalisha mbegu za zao hilo mkoani hapa kwa kuwa nchi ina wataalamu wa kutosha wa kilimo.

"Nchi nzima mzalishaji wa mbegu ya viazi mviringo ni mmoja kwa hiyo siku akiamka akakwambia amepoteza interest ya kuzalisha mbegu Tanzania tumekufa," alisema Mtaka.

## Wafanyakazi waendelea kugoma kushinikiza kulipwa mishahara

**Na Mwandishi Wetu,** NJOMBE

WAFANYAKAZI wa Kiwanda cha chai cha DL Kibena wameingia siku ya saba kwenye mgomo wa kuingia kazini kwa madai ya kushinikiza kulipwa malimbikizo ya mishahara ya miezi minne.

Wakizungumza na waandishi wa habari, nje ya kiwanda hicho, walidai uongozi wao haujawalipa mishahara yao kwa kipindi hicho na kushindwa kumudu gharama za maisha.

Mmoja wa Wafanyakazi hao, Chesco Mligo, aliiomba serikali kuingilia kati na kuhakikisha wanalipwa mishahara hiyo ili wamudu kuendesha maisha yao.

"Tunazungumza hili kwa uchungu kwa sababu tangu huyu mwekezaji amefika sisi ni watu wa kulia tu licha ya kumpandia chai na biashara anafanya," alidai Mligo.

Kalorina Komba, alidai kutolipwa mishahara hiyo kumesababisha washindwe kumudu mahitaji ya familia kwa kukosa fedha.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi Mashambani nchini (TPAU) Tawi la kiwanda hicho, Elisha Mbembati, alisema kuwa mwajiri huyo amelipa mshahara wa mwezi mmoja na kuwaomba wafanyakazi hao kurejea kazini na kuahidi kuendelea kulipa.

Katibu wa TPAU wa tawi hilo, Frida Kidenya alisema mwajiri huyo pia hajawasilisha michango ya wafanyakazi kwenye Shirika la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kwa muda wa miaka sita.

Meneja wa Kiwanda hicho, Geradi Ng'enzi, alithibitisha wafanyakazi hao kudai malimbikizo hayo ya mishahara na kuahidi kuendelea kulipa kadri fedha zitakapo patikana walau kwa mwezi mmoja.



Kaimu Mkuu wa Polisi Jamii mkoa wa Simiyu, Mkaguzi wa Polisi, Francis Msuku, akitoa elimu kuhusu haki za msingi za raia kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Biashara, Gambosi, mkoani humo juzi. Kushoto ni Katibu Mkuu wa Shirika la Kutetea Haki za Abiria (SHIKUHA), Hashim Omary. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Halmashauri zaagizwa kuanzisha Kliniki ya Mama Samia

**Na Mwandishi Wetu,** NJOMBE

SERIKALI mkoani hapa imeziagiza halmashauri kuanzisha kliniki ya Mama Samia ili kumaliza vikwazo na adha kwa walimu na kuinua kiwango cha taaluma shuleni.

Agizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka wakati akifungua Kliniki ya Mama Samia kwa lengo la kusikiliza na kutatua kero sugu za walimu.

Kissa, alisema kuna umuhimu wa kutenga siku za kutatua kero za walimu kutokana na idadi kubwa ya waliojitokeza wakiwemo wastaafu ili kupatiwa ufumbuzi wa kero zinazokwamisha utekelezaji wa majukumu yao.

"Ningeomba hata maofisa utumishi mliopo hapa muweke utaratibu kwenye wilaya zenu na kila halmashauri kuwafuata walimu kwenye tarafa na kata zao, kwa wingi huu unanieleza walimu wanachangamoto," alisema.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameweza kutatua kero nyingi ikiwemo kutoa madaraja kwa mserereko.

Awali akizungumza kilichowasukuma kuja na programu hiyo, Makamu wa Rais wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Suleiman Ikomba, alisema mrundikano wa matatizo ya walimu umewasukuma kumiminika kwenye kliniki hiyo ili kuboresha mazingira ya kazi na kuonya wanaokivuruga chama hicho.

"Ukipuuza, ukiwatendea makosa watumishi wa umma ambao wanafanya kazi kwa kumuwakilisha Rais Samia unawakosea, na umeikosea ilani ya chama inayotokana na wakati huo," alisema Ikomba.

Baadhi ya walimu ambao wamefika kwenye kliniki hiyo akiwemo, Henrick Nehemia, alisema kitendo cha kuunda timu ya wataalamu kuwafuata walimu mikoani kusikiliza kero zao, kimewapunguzia usumbufu na gharama ya kufuata huduma hizo mkoani Dodoma.

Kliniki hiyo imehusisha wataalamu kutoka wizara za elimu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na utumishi kufuatia kundi kubwa la walimu kujitokeza kuwasilisha malalamiko.

Njombe ni mkoa wa 10 kufikiwa na kliniki hiyo ya Mama Samia.

# Watakiwa kudhibiti uvuvi haramu

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WASIMAMIZI wa hifadhi za bahari visiwani hapa wametakiwa kudhibiti uvuvi haramu katika maeneo yao kuwa ndio wasimamizi kwa kutumia sheria.

Meneja wa Hifadhi ya Ghuba ya Menai, Dk. Than Rashid Said, alitoa rai hiyo jana wakati wa mafunzo ya kinadharia na vitendo juu ya ufanyaji wa doria na usimamizi wa sheria za uvuvi baharini yanayofanyika Maruhubi.

Dk. Said, alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa wasimamizi hao kutokana na kukithiri kwa uvuvi haramu kwa baadhi ya maeneo na kurudisha nyuma juhudi za serikali.

Alisema mafunzo hayo yamewajengea uwezo wa kufanya kazi kwa weledi na ustadi.

Mshauri wa Shirika la Uhifadhi la Wanyamapori Tanzania (WCS), Noah Mpunga, alisema WCS inaleta miradi mbalimbali kwa wananchi kwa ajili ya utanzaji mazingira ya bahari bila ya kuathiri jamii.

Mpunga, aliwataka wanufaika wa mafunzo hayo kushirikiana na jamii kwa kutumia kanuni za uhifadhi wa bahari ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Washiriki wa mafunzo hayo, walisema yatawasaidi kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazotokea wakati wa usimamizi wa rasilimali hizo za bahari.

Wataalamu wa mafunzo hayo, akiwemo Hyasint Donald Wariri na Haji Machano Ali wa Chuo cha Feta Mbegani Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani, walisema ili kuwe na maendeleo nchini lazima kuwe na wasimamizi wa sheria za uvuvi baharini kwa ajili ya kutunza mazingira na rasilimali za bahari.

Waliwataka wakufunzi wa mafunzo hayo kuzingatia taaluma kutokana na sera ya uchumi wa buluu Zanzibar kuwa chachu ya maendeleo kwa jamii na taifa.

**Dk. Said, alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa wasimamizi hao kutokana na kukithiri kwa uvuvi haramu kwa baadhi ya maeneo na kurudisha nyuma juhudi za serikali.**

# Wananchi wahamasishwa kujiunga bima ya afya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MFUKO wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF) umeanza kuhamasisha usajili wa wananchi wa kundi la sekta isiyo rasmi ili kuhakikisha wanapata huduma za bima ya afya visiwani hapa.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko huo, Yassir Juma wakati akizungumza na wananchi, wafanyakazi wasio katika sekta rasmi, wafanyabiashara na wajasiriamali katika kampeni za kuhamasisha usajili wa mfuko.

Juma, alisema mfuko huo umeanzishwa na Serikali ya Zanzibar kwa sheria namba moja ya mwaka 2023 iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi.

Alisema katika kufikia malengo hayo, mfuko huo umedhamiria kuyafikia makundi yote ili kuhakikisha yanapata huduma sawa za afya.

"Tumekamilisha kufanya usajili kwa watumishi wa Serikali ya Mapinduzi ambao wapo katika mfumo rasmi kwa asilimia 80 na sasa tunaingia sekta isiyo rasmi ili kutimiza malengo ya upatikanaji wa huduma za afya kwa wote," alisema.

Mkurugenzi wa Uratibu wa Mfuko huo, Juma Hamad, alisema kazi ya kusajili watumishi wa serikali imekwenda vizuri.

Hamad, alisema waliosalia ni wachache ambao baadhi yao taarifa hazijaingizwa katika mfumo rasmi wa mtandao.

Alisema usajili sekta rasmi ulianza Julai mwaka juzi na kwamba watumishi wa serikali wanatakiwa kuchangia mfuko huo kwa asilimia 3.5 ya mshahara.

Akitoa tathmini ya usajili huo, alisema umefanyika kwa mafanikio makubwa baada ya mfuko huo kupata ushirikiano mzuri kutoka kwa maofisa utumishi wa wizara na taasisi zake.

Hamada, alisema hospitali zote zinatakiwa kutoa huduma za bima ya afya kwa watumishi hao wa serikali wakati zoezi hilo linaendelea.



Wauzaji wa mchanganyiko wa vipande vya mihogo, nazi na karoti maarufu kama vifurushi, wakiandaa bidhaa zao, katika eneo la Tabata, jijini Dar es Salaam jana, kabla kuingia mitaani kusaka wateja. **PICHA: BEATRICE MOSES**

# Mahakama Kuu kuendesha mashauri kidigitali

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAHAKAMA Kuu ya Zanzibar imesema mashauri yote yanatarajiwa kuendeshwa kwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Hayo yalisemwa na Jaji Mkuu wa Zanzibar, Khamis Ramadhan Shaaban wakati akitambulisha mradi wa maboresho ya mahakama hiyo kwa majaji, mahakimu na wadau katika mfumo wa haki jinai.

Shaaban, alisema mradi huo unakwenda sambamba na Malengo Dira ya Maendeleo ya mwaka 2050 katika utawala bora, uwajibikaji na kufikiwa kwa malengo endelevu ya dunia katika upatikanaji wa haki.

Alisema mahakama ni nguzo muhimili ya upatikanaji wa haki katika mfumo wa dunia, hivyo wanatakiwa kwenda na wakati wa mabadiliko ya sasa na yanayoendelea kutokea.

Alisema hatua hiyo, itakidhi mahitaji ya wananchi na kuondoa manung'uniko yasiyokuwa na msingi miongoni mwao.

Jaji wa Mahakama Kuu, Ibrahim Mzee, alisema mradi huo kati ya malengo yake ni kuleta mageuzi makubwa ya kutoa huduma.

Mzee, alisema kwa sasa wanaingia katika mfumo wa kidigitali wa matumizi ya TEHAMA kutoa haki kwa wananchi.

Alisema kwa sasa mahakama zote na watendaji wake wanaondoka katika mfumo wa matumizi ya karatasi kutoa haki na taarifa zake.

Alisema mfumo huo utasaidia kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa taarifa, takwimu za mwenendo wa usikilizaji wa mashauri katika mahakama na kuondokana na urasimu wa ucheleweshaji kesi kitendo ambacho kinawaumiza baadhi ya wananchi.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mtendaji Mkuu wa Mahakama Kuu nchini, Profesa Elisante Ole Gabriel, alisema wakati umefika kwa Mahakama Kuu ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano kushirikiana katika majukumu na kuimarisha utoaji haki kwa wananchi.

Baadhi ya majaji wameunga mkono maboresho hayo ambayo lengo lake ni kuendesha mashauri yanayowasilishwa na wananchi kwa wakati na haki kutendeka.

" Mageuzi katika mfumo wa uendeshaji mahakama zetu hauepukiki kwa sasa umelenga kuhakikisha wananchi wanapata haki katika usikilizwaji wa mashauri yao kwa wakati," alisema Jaji Aziza Suwedi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**ATIA EDSON SUGAVAKI**, anatangaza kupotea kwa Cheti cha Kidato cha Nne chenye Index namba **S1409/0002** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **Shule ya Sekondari HAGAFILO** Mwaka 2022. Yeyote atakayekiona atoe taarifa Kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi **:PHQ/DAR/TEM/14226/2025**

## KUPOTEA KWA CHETI



**PIUS M COSMAS** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index **No. S0880-0090** Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KAIGARA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/SHI/SHI/6219/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SALMA IDD MBOGO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye **index namba S0738-0507** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **RIDHWAA SEMINARY** mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/TEM/16266/2025.**

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**DEEP POLL**
**CHANGE OF NAME**
**(THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT (CAP.117.R.E 2002)**

**I, THERESIA JOHN KINYAIYA** a Tanzanian, Christian, adult of P.O. Box 516, MOSHI, formerly known as **THERESIA JOHN KISSOLY, I** do hereby absolutely renounce and abandon the use of my former name of **THERESIA JOHN KISSOLY** and in lieu thereof I assume and adopt the name of **THERESIA JOHN KINYAIYA**

I absolutely and entirely **RENOUNCE RELINQUISH and ABANDON** the use of my former name **THERESIA JOHN KISSOLY** as it appears to my pension Identity with SSN: 4424860 and in lieu thereof do assume the name of **THERESIA JOHN KINYAIYA** as it appears to my National Identity card No. **19581002-25113-00003-16.**

And in pursuance of such change of name as aforesaid I hereby declare that I shall at all time hereinafter in all Records Deeds and Instruction in writing and in all actions and proceedings and in all dealings and transactions and upon all occasions whatsoever use and sign the said name **THERESIA JOHN KINYAIYA** as my name in lieu of the said **THERESIA JOHN KISSOLY** renounced as aforesaid.

**AND I HEREBY AUTHORISE AND REQUEST** all persons to designate and address me in the name of **THERESIA JOHN KINYAIYA**

I, **THERESIA JOHN KINYAIYA** make this Declaration conscientiously believing the same to be true and in accordance of the provision of the Oaths (Judicial Proceedings) and Statutory Declaration Act (Cap 34 R.E 2019)

AFFIRMED and DELIVERED at Arusha by the said **THERESIA JOHN KINYAIYA** who is known to me personally / identified to me by........................ this ....9.....day of...JANUARI.....2025.

..................
**DEPONENT**



**BEFORE ME:**
**NAME:** ...JOSEPH PETER...
**SIGNATURE:** ..............
**ADDRESS:** ...1517 - MOSHI...
**QUALIFICATION: COMMISSIONER FOR OATHS**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EVERINA ANDREW MASSAWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 566 AYG – HIACE SUPER CUSTOM** yenye jina la umiliki wa **ANDREW ELIKANA NATHAN.** Yeyote akatayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi: **PHQ/MBE/MBE/2793/2025.**

## KADI ZA PIKIPIKI ZIMEPOTEA

Ndugu **JOSEPH VENCESLAUS SHAYO** anatangaza kupotelewa kwa kadi mbili za pikipiki zenye namba za usajili. **MC 905 CDX** yenye Engine Namba: **G7157FMIJZA80057.** Pamoja na **MC 773 DCZ** yenye Engine Namba: **G7157FMIM5A80338.** Kwa yeyote atakayeziona anaombwa kutoa taarifa kwenye kituo chochote cha Polisi kilicho karibu. Taarifa Polisi: **PHQ/TAN/TAN/683/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MASHAKA MANENO JUMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 676 AEJ** aina ya Honda, Chasis namba **MD03-1008841,** Engine namba **MD03E-1008849.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/MAN/BAB/254/2025**

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI

**ODILIA ALPHONCE TARIMO** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC 560 BVT.** Chasses Namba **MD6M14PK1H4L11110,** Engine Namba **OK4LH4435801.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . Polisi Taarifa : **PHQ/KIL/MOS/494/2025**

## KADI ZA PIKIPIKI ZIMEPOTEA

Ndugu **RAMADHANI ALLY MGUNDUZI** anatangaza kupotelewa kwa kadi mbili za pikipiki zenye namba za usajili. **MC 758 CRX,** pamoja na **MC 881 APF.** Kwa yeyote atakayeziona anaombwa kutoa taarifa kwenye kituo chochote cha Polisi kilicho karibu. Taarifa Polisi: **PHQ/TAN/TAN/727/2025.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya Shinyanga**

**Kituo cha Mjini na Mkoa Shinyanga**

**Shauri la Madai Na112/ 2024**

**Jina la Mdai: Shinyanga Municipal Warkers Saccos**

**Jina la Mdaiwa: Mbuke .M. Maduhu**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 kanuni za taratibu madai katika Mahakama ya Mwanzo)**

**Kwa Mbuke .M. Maduhu wa Shinyanga**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake ya Tshs.5,716,000/-
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 21 mwezi 01 mwaka 2025 saa 8.30 asubuhi
kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta ushahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**Angalizo:** kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa na Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 15 mwezi wa 01 mwaka 2025

SAHIHI YA MPOKEAJI..........
SAHIHI YA MWASILISHAJI..........
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
SHINYANGA

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.31348 OF 2024**

**IN the Matter of the late: MARKO JOSEPHAT NSIMBI**

1. FRORAH ADALABERT NTWALAMANI
2..........................................

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above- named pepetitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 22 day of 01,2025.
Dated at Morogoro this 27 day of 12, 2024.

..................................
RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA**
**AT KYELA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 1218 OF 2025.**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ASWILE ANDINDILILE MWAKILIMA**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY ANESTER ASWILE MWAKILIMA..............PETITIONER**

**GENERAL CITATION (RULE 75)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 06 day of February, 2025.

Dated at Kyela Mbeya this 17 day of January, 2025.

..................
*SENIOR RESIDENT MAGISTRATE*
*KYELA.*

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/ PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701
AU
TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO,MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Trump aahidi kutoa amri za kiutendaji

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS mteule wa Marekani Donald Trump ameahidi kusaini amri ya utendaji katika siku yake ya kwanza kama rais, akiwaeleza wafuasi wake kwamba atasonga mbele kwa kasi ya kihistoria na nguvu katika saa chache baada ya kula kiapo.

Akihutubia umati mkubwa wa maelfu ya watu katika uwanja wa Washington DC jana Trump alitoa hakikisho la miaka minne ijayo na kusherehekea ushindi wake wa uchaguzi wa mwezi Novemba dhidi ya Democrats.

Chama cha Republican kiliahidi kuchukua hatua bila kuhusisha chama kingine katika masuala mbalimbali, kwa kutumia mamlaka yake ya urais kuanzisha operesheni za kuwarudisha watu wengi katika nchi zao, kupunguza kanuni za mazingira na kusitisha mipango inayowahusu watu wa jamii mbali mbali.

"Tunaiweka Marekani kwanza na yote yanaanza kesho, 'leo' kila amri ya kiutendaji yenye msimamo mkali na ya kijinga ya utawala wa Biden itafutwa ndani ya saa chache baada ya kuapishwa," rais huyo anayeingia mamlakani alisema.

Trump aliahidi kuweka amri za kiutendaji ambazo zitaimarisha mipango ya akili mnemba (AI), kuunda Idara ya Ufanisi wa Serikali, kukusanya rekodi zinazopatikana kuhusiana na mauaji ya John Kennedy mnamo 1963, kuelekeza jeshi kuunda ngao ya ulinzi wa makombora ya Iron Dome.

Pia aliwaambia wafuasi wake kuwa atawazuia wanawake waliobadili jinsia kushindana katika makundi ya michezo ya wanawake na kurudisha udhibiti wa elimu kwa majimbo ya Marekani.



"Utaona maagizo ya kiutendaji ambayo yatakufanya uwe na furaha sana. Tunapaswa kuweka nchi yetu katika njia sahihi," alisema. **BBC**

# Vita Gaza vyasitishwa rasmi Wapalestina 90 waachiliwa

**JERUSALEM,** Israel

ISRAEL imewaachilia wafungwa 90 wa Kipalestina waliokuwa katika gereza la Ofer lililopo katika eneo la Ukingo wa Magharibi, baada ya Hamas kuwaachilia mateka watatu wa Israel na kukamilisha mabadilishano ya kwanza chini ya mpango wa kusitisha vita.

Wafungwa hao waliachiwa jana na Israel, baada ya Hamas huko Ukanda wa Gaza kuwaachia waisraeli watatu juzi ambao wote ni wanawake na tayari wameungana na familia zao baada ya kupelekwa hospitali kuchunguzwa afya zao, na kwamba madaktari walisema wote watatu wapo katika hali nzuri ya kiafya.

Kansela wa Ujerumani Olaf Scholz alisema kuanza kwa mabadilishano hayo kunatoa matumaini kwamba mateka wengine pia wataachiliwa.

Katika mpango wa makubaliano ya awali ni kwamba jumla ya mateka 33 wa Israel, wanatarajiwa kurejeshwa kutoka Gaza. Na kwamba 31 kati yao ni wale waliochukuliwa na wanamgambo wa Hamas wakati wa mashambulio ya Oktoba 7, 2023. Huku ikielezwa kuwa Israel itawaachia wafungwa wa Kipalestina wapatao 1,900.

### WAREJEA MAKWAO

Ilielezwa kuwa baada la hatua hiyo, vita vimesitishwa rasmi hali iliyoibua matumaini mapya kwa maelfu ya Wapalestina ambao wameanza kurejea makwao baada ya Israel na Hamas kuanza utekelezaji wa makubaliano ya usitishaji vita.

Ilibainishwa kuwa kuchelewa kwa hatua ya usitishaji vita kulitokana na mvutano uliozuka kuhusu orodha ya mateka wa mwanzo watakaoachiliwa chini ya mpango huo na kundi la Hamas.

Qatar ambayo ni mpatanishi kwenye makubaliano hayo ilithibitisha kwamba kundi la Hamas hatimae lilitoa orodha ya majina ya raia wa Israel watakaoachiliwa huru na kwamba sasa utekelezaji wa makubaliano hayo umekwishaanza rasmi.

Awali ofisi ya Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu ilisema kwamba hatua ya awali ya usitishaji mapigano kwa wiki sita itaanza kutekelezwa saa 11.15 asubuhi.

Licha ya usitishaji huo mapigano kuwa na mwanzo uliokabiliwa na kizingiti, Wapalestina walionekana kusherehekea katika maeneo mbali mbali yaliyokabiliwa na vita vya muda mrefu huku maelfu yao wakionekana kuanza kurejea majumbani kwao.

Makubaliano hayo ni hatua ya kwanza kuelekea kumalizwa kabisa kwa vita katika eneo hilo na kuachiliwa kwa mateka takriban 100 waliotekwa nyara na kundi la Hamas katika uvamizi wao huko Israel, Oktoba 7, 2023, uliochochea vita vya Gaza.

Wakati huohuo Waziri wa Usalama wa wa Israel kutoka chama cha mrengo mkali wa kulia Itamar Ben-Gvir alijiuzulu nafasi yake, kama hatua ya kupinga kusitishwa kwa mapigano kati ya Israel na Hamas katika Ukanda wa Gaza. **DW**



Miongoni mwa raia wa Palestina wanaoishi katika ukanda wa Gaza wakirudi katika makazi yao waliyoyakimbia baada ya vita kati ya Israel na Hamas kusitishwa rasmi jana. **PICHA: MTANDAO**

# Wizara yaomba mawakili wasitozwe ushuru

**KAMPALA,** Uganda

WIZARA ya Sheria na Mambo ya Katiba nchini Uganda, imeomba bunge kuwaruhusu mawakili wa serikali kutolipa kodi ya mapato ili kupunguza pengo la tofauti ya mishahara kati ya mawakili wa serikali na wenzao waendesha mashtaka katika Ofisi ya Kurugenzi ya Mashtaka (ODPP) na Mahakama.

Waziri wa Sheria, Nobert Mao alisema jana kuwa ofisi ya DPP haikabiliwi na tatizo kama hilo kwa sababu wameondolewa ushuru wa mapato, hivyo wanapata malipo bora.

"Tunataka hivyo hivyo kwa Mawakili wa Wizara ya Sheria ili nao wapewe malipo ya ushindani na waache kutafuta kazi nje. Kila mwaka, tunapoteza baadhi ya mawakili wetu bora na bado tumewekeza katika kuwafundisha na ghafla, wanaenda Mahakama Kuu kwa sababu sheria na masharti ni bora zaidi. Hii inaathiri ubora wa kazi zetu," alisema Mao.

Fox Odoi mbunge wa Budama Kaskazini bado anazungumza juu ya tofauti ya malipo kwa kazi hiyo hiyo, wakati yeye mwenyewe anakaa kwenye Baraza la Mawaziri ambalo linakuja na sera hizo.

"Tunaongelea mwaka 2025, Waziri anasema kuwa ana wanasheria katika ODPP ambao wanalipwa zaidi ya wanasheria wa serikali, kazi sawa, malipo tofauti," Odoi alisema.

Wakati huo huo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema timu yake ilishinda kesi 311 mahakamani na hapo serikali ikaokoa zaidi ya dola milioni 758 (Sh. Trilioni 1.9)

Alisema serikali pia ilipoteza kesi 101 zenye thamani ya zaidi ya dola milioni 48 (Sh. Bilioni 120.9) mwaka 2024.

Katibu Mkuu Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba ya Uganda Robert Kasande, alisema "Pia tuliweza kuitetea serikali katika kesi 180 za kikatiba, rufaa na maombi katika Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki".

Hata hivyo, Jonathan Odur mbunge wa Erute Kusini aliitaka Wizara kueleza ni kiasi gani cha fedha kwa kesi iliyoshindwa zimerejeshwa na serikali.

"Serikali imeshinda kesi nyingi, inapata mapato kutokana na juhudi hizo kwa sababu watu wameishtaki serikali imeshindwa, kwao wanapokea malipo ya fidia. Tunataka kuona takwimu za mapato yenu," Odur alisema. **TRT**

HABARI MICHEZO

# KIPENGA LIGI KUU Z'BAR DURU LA PILI CHAPULIZWA

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LIGI Kuu Zanzibar mzunguko wa pili inatarajia kurejea mwisho mwa mwezi huu baada ya kusimama kwa muda kupisha michuano ya Kombe la Mapinduzi, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Issa Kassim, alisema ratiba ya ligi hiyo inatarajiwa kutolewa kuanzia ndani ya wiki hii.

**Alisema tayari taarifa ya kurejea kwa ligi hiyo imeshafikishwa kwa klabu zote 16 za Ligi Kuu Zanzibar kutoka Unguja na Pemba.**

Kuhusu viwanja vitakavyotumika kwa ligi hiyo, alisema kwa upande wa michezo itakayochezwa Kisiwani Pemba itaendelea katika uwanja wa Finya kutokana na ule wa Gombani kuendelea kufanyiwa ukarabati.

Kwa Unguja, alisema ligi hiyo itachezwa kwenye Uwanja wa Mau ambao kwa mujibu wa idara ya michezo, upo katika hatua ya mwisho ya ukarabati.

"Ratiba tunatarajia kuitoa muda wowote kuanzia sasa, tulisita kuandaa ratiba mapema kwani awali tulitarajia CHAN (Michuano ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani), kuanzia mwezi ujao," alisema Kassim.

Aidha, alisema bodi hiyo kupitia Kamati ya Kusimamia na Kuendesha Ligi, inaendelea na maandalizi yake kuelekea michezo hiyo ya mzunguko wa lala salama.

"Kama tunavyojua mzunguko huu tunatakiwa kuwa macho sana, kwani ndio ambao tunaenda kupata bingwa, lakini ni mzunguko ambao kila mmoja anapambana ili kupata nafasi ya kubaki Ligi Kuu," alisema.

Ligi Kuu Zanzibar ambayo inadhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), kinara wa ligi hiyo hadi mzunguko wa kwanza ulipokamilika, ni Mlandege FC yenye alama 30, huku nafasi ya pili ikikaliwa na Mafunzo FC na alama zake 27 sawa na Muembe Makumbi City ambayo ipo nafasi ya tatu.

FUNGA KAZI...




Mshambuliaji wa Simba, Elie Mpanzu, akijaribu kuifungia timu yake bao wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya CS Constantine ya Algeria kwenye mechi ya Kundi A Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Mserbia aapa kuibakisha KenGold Ligi Kuu*

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA mpya wa KenGold, Mserbia Vladislav Heric, amewahakikishia mashabiki wa timu hiyo kuwa timu hiyo haitoshuka daraja na amekuja kwa kazi moja tu ya kuhakikisha inabaki Ligi Kuu.

Akizungumza kwa mara ya kwanza jana baada ya kutangazwa kuwa kocha wa timu hiyo hivi karibuni, Heric, amesema amefurahi sana kujiunga na timu hiyo, ingawa imeikuta iko chini ya msimamo wa Ligi Kuu, lakini huwa anapenda sana ushindani, hivyo anaamini ataiokoa kwenye janga hilo.

"Nimefurahi kujiunga kwenye klabu hii, napenda sana ushindani, naamini nitaiokoa timu kwenye hatari ya kushuka daraja, na hii ndiyo kazi yangu, nimeshaifanya sana klabu nilizotoka.

"Nitakaa na kikosi changu na kuangalia nini cha kufanya kwenye uwanja wa mazoezi. Lakini hili haliwezi kuwa peke yangu, ni lazima kila mmoja wetu awajibike, kuanzia dereva, mashabiki, wachezaji, bendi la ufundi hadi mabosi wa klabu," alisema kocha huyo, raia wa Serbia.

Alisema kwake muda si tatizo sana, ila anachohitaji ni ripoti ya kilichofanyika mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu, ili ajue wapi kwa kuanzia.

"Muda siyo muhimu kwangu, nataka kuondoa matatizo yaliyopo, nahitaji ripoti ya nini kilifanyika mzunguko wa kwanza ili nijue nianzie wapi. Tunahitaji kubadilisha kila kitu hadi mazingira, tunahitaji kuwaomba msamaha mashabiki kutokana na matokeo mabovu kabla ya kuanza upya.

Kabla ya kutua KenGold, kocha huyo amezifundisha Klabu za Chippa United na Cape Town za Afrika kusini.

KenGold, ambayo imesajili jumla ya wachezaji 22 kipindi cha uhamisho wa dirisha dogo, inaburuza mkia mpaka kumalizika kwa mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu, ikiwa na pointi sita tu kwa michezo 16 iliyocheza, ikishinda mmoja, sare tatu na kupoteza mechi 12.

# Kocha Azam atoa sababu kibao kichapo Mtibwa Sugar

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Azam FC, Rachid Taoussi, amesema kukaa kwa wiki tatu na nusu bila kucheza mechi pamoja na kuwatumia wachezaji wengi waliokuwa majeruhi na wapya waliosajiliwa kipindi cha usajili wa dirisha dogo ndiyo sababu iliyowafanya kupoteza kwa bao 1-0 dhidi ya Mtibwa Sugar juzi.

Ikiwa kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Turiani mkoani Morogoro, Azam ilijikuta ikiambulia kipigo cha bao 1-0 lililofungwa na straika hatari, anayeongoza kwenye ufungaji wa mabao kwenye Ligi ya Championship, akiwa na mabao 11, Raizin Hafidh, alilolifungwa kwa mkwaju wa penalti baada ya yeye mwenyewe kubwagwa ndani ya 18, katika mechi ya kujipima nguvu.

"Ni mchozo wetu wa kwanza baada ya kukaa wiki tatu na nusu bila kucheza mechi yoyote baada ya ligi kusimamishwa, tuliwapa wachezaji wetu muda wa kupumzika na sasa ndiyo wamerudi, wasingeweza kuwa na kiwango ambacho walimaliza nacho kwenye mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu.

"Na wengi katika mchezo huu niliwapa dakika kadhaa za kucheza na si zote, nimewachezesha wachezaji wengi ambao walikuwa majeruhi kwa muda mrefu, na wale wapya ambao wamesajiliwa kipindi hiki cha dirisha dogo, bado hawajaelewana na wenzao, hivyo kazi ilyopo ni kusaka muunganiko," alisema kocha huyo raia wa Morocco.

Pamoja na hayo, kocha huyo alisema aliwafanyisha wachezaji wake mazoezi magumu, hivyo bado walikuwa kwenye uchovu.

"Kingine ni kwamba tulikuwa na mazoezi magumu sana kwa siku mbili, ambayo yalihusisha utimamu wa mwili, wachezaji wangu bado wana uchovu mkubwa, nahitaji muda tena," alisema.

Hata hivyo, alisema matokeo kwake si muhimu, bali ni kile alichokiona kwa wachezaji wake, ambapo anadai walijitahidi kucheza vema, ingawa makosa madogo ikiwamo kusababisha penalti, kuliwagharimu.

Aliisifu Mtibwa Sugar kuwa ni moja kati ya timu ngumu, akisema wamepata kipimo sahihi, akiitabiria kurejea Ligi Kuu msimu ujao.

"Nashukuru tumepata mechi nzuri, ngumu na yenye ushindani kutoka kwa timu ambayo inaongoza Ligi ya Championship, Mtibwa Sugar msimu uliopita ilikuwa Ligi Kuu, na haijapoteza ubora wake kwenye ligi iliyokwenda, nina uhakika msimu ujao tutakuwa nao tena huku juu,"alisema Taoussi.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### DOUGLAS ATAKIWA CITY

KLABU ya Manchester City inafikiria kumsajili kwa mkopo kiungo wa Brazil, Douglas Luiz mwenye umri wa miaka 26, ingawa Juventus inashinikiza usajili wa kudumu. ***(Athletics)***

### VINICIUS AWANIWA SAUDIA

KLABU za Ligi Kuu Saudi Arabia bado zina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Real Madrid, Vinicius Jr mwenye umri wa miaka 24, nchini humo - huku mtendaji mkuu wa ligi hiyo akisema usajili wake ni "suala la muda tu". ***(ESPN)***

### CHALOBAH PAUNI MILIONI 40

CHELSEA inataka pauni milioni 40 kumuachia beki, Trevoh Chalobah, baada ya kumrejesha mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 25 kutoka Crystal Palace. ***(Sun)***

### CASADEI ANUKIA LAZIO

NYOTA wa Chelsea, Cesare Casadei mwenye umri wa miaka 22, huenda akaelekea Lazio baada ya klabu hizo mbili kukaribia kuafikiana. ***(Sky Sports Italia)***

### ANTONY HUYOOO REAL BETIS

MECHI ya juzi Jumapili ya Man United dhidi ya Brighton ilikuwa ni ya mwisho kwa winga wa Brazil, Antony, 24, akiwa amevalia jezi ya klabu hiyo, baada ya makubaliano ya awali kuhusu uhamisho wake wa mkopo kuelekea Real Betis. ***(Fabrizio Romano)***

### TEN HAG NA DORTMUND

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Erik ten Hag, anaweza kuchukua nafasi ya Nuri Sahin kama kocha wa Borussia Dortmund ikiwa klabu hiyo itashindwa katika mechi yao ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Bologna leo, Jumanne. ***(Florian Plettenberg, Sky Sports Germany)***

### GITTENS SASA AGOMBEWA

KLABU za Manchester United na Chelsea zitachuana na Bayern Munich kuwaniwa kumsajili kiungo wa England, Jamie Gittens, 20, dirisha la majira ya kiangazi. ***(Florian Plettenberg, Sky Sports Germany)***

### DAVIES BASI TENA

REAL Madrid iko tayari kusitisha nia yao ya kumsajili beki wa Canada, Alphonso Davies, 24, ambaye anakaribia kufikia makubaliano ya kuongeza mkataba wake pale Bayern Munich. ***(AS)***

### KELLY ATAKIWA JUVENTUS

JUVENTUS ina nia ya kusajili mlinzi wa Newcastle United, Lloyd Kelly, 26, - miezi saba tu baada ya mchezaji huyo kuwasili kutoka Bournemouth kwa uhamisho wa bure. ***(Gianluca di Marzio)***

### BARRY MKATABA MPYA

ASTON Villa imeanza mazungumzo na kiungo wa England, Louie Barry mwenye umri wa miaka 21, kuhusu mkataba mpya huku Celtic wakionesha nia ya kutaka kumsajili. ***(Football Insider)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE RASMI AKIRI KUIZOEA REAL MADRID

**MADRID,** Hispania

KYLIAN Mbappe amekiri kuwa sasa yuko karibu na ubora wake baada ya kufunga mabao mawili katika ushindi wa 4-1 wa Real Madrid dhidi ya Las Palmas Jumapili, akisema "sasa nimeizoea timu, na ninaweza kucheza ninavyotaka."

**Madrid walianza kuwa nyuma katika dakika ya kwanza kwenye Uwanja wa Bernabeu, kabla ya Mbappe kusawazisha kwa mkwaju wa penalti, Brahim Diaz akaongeza la pili, na Mbappe akafunga la tatu, huku jingine likikataliwa kwa kuotea.**

Rodrygo alifanya matokeo kuwa 4-1 katika kipindi cha pili, huku Jude Bellingham na Federico Valverde wote mabao yao yakikataliwa na VAR, na sasa Madrid wapo mbele kwa pointi mbili kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

"Nina furaha sana," alisema Mbappe akiiambia Real Madrid TV, alipoulizwa kuhusu umati wa mashabiki kwenye Uwanja wa Bernabeu kuimba jina lake wakati wa mchezo huo.

"Nimezoea timu sasa na ninaweza kucheza ninavyotaka, na wachezaji wenzangu. Sote tunafurahia."

Mbappe alikabiliwa na ukosoaji mapema msimu huu, lakini sasa amefunga mabao 18 katika mashindano yote, yakiwamo manne katika mechi tatu za mwisho wiki hii.

Ushindi wa Madrid ulikuwa wa kuchukua fursa nzuri baada ya Atletico Madrid kupoteza kwa bao 1-0 dhidi ya Leganes - na Barcelona, ambao walitoka sare ya 1-1 na Getafe.

"Ulikuwa mchezo muhimu, tulijua kilichotokea jana (juzi), tulijua Atletico na Barcelona hawakuwa na matokeo mazuri," alisema Mbappe.

"Tulitaka kushinda, na tulifanya mambo yawe mazuri. Tulianza vibaya ... lakini majibu yalikuwa 'juu'.

"Tulikuwa kwenye mguu wa mbele, tukicheza kwa kasi, tukishambulia nafasi kwa ubora. Tulifunga mabao mengi. Tuna furaha, kwa sababu sisi ni viongozi."

Ushindi dhidi ya Las Palmas ulikuwa jibu nzuri baada ya kufungwa mabao 5-2 na Barcelona kwenye fainali ya Supercopa ya Hispania, na kuhitaji muda wa ziada kuifunga Celta Vigo katikati ya wiki kwenye Copa del Rey.

"Ninajivunia majibu ya [timu]," alisema Mbappe.

"Kupoteza Supercopa ilikuwa ngumu, na ingawa tulicheza vizuri kwenye kombe, tulifanya makosa na kwenda kwenye muda wa ziada. Lakini tulikuwa na utu wa kushinda. Leo (juzi) ilikuwa muhimu sana. Sasa tunategemea kushinda ligi."

> Nina furaha sana, sasa ninaweza kucheza ninavyotaka na wachezaji wenzangu, najivunia...

HABARI MICHEZO



# MAN UNITED HALI YAZIDI KUWA MBAYA

**MANCHESTER,** England

RUBEN Amorim amesema timu yake ya Manchester United huenda ikawa mbaya zaidi katika historia ya klabu hiyo baada ya kufungwa mabao 3-1 na Brighton & Hove Albion, Jumapili.

United ilishindwa kusajili shuti lililolenga lango katika mchezo huo huku Brighton wakitawala pale kwenye dimba la Old Trafford.

Matokeo hayo yanamaanisha kuwa Amorim tayari amepata vipigo vinne vya Ligi Kuu ya England nyumbani tangu achukue timu kama kocha mkuu kutoka kwa Erik ten Hag, ambaye alitimuliwa mwishoni mwa Oktoba.

"Tunapata kocha mpya ambaye anapoteza zaidi ya kocha aliyepita," alisema Amorim

"Nina ufahamu kamili wa hilo. Najua tunaweza kufanikiwa, lakini tunahitaji kunusurika wakati huu.

"Tunahitaji kunusurika sasa. Sisi ni timu mbaya zaidi, labda, katika historia ya Manchester United.

"Najua mnataka vichwa vya habari, lakini nasema hivyo kwa sababu tunapaswa kukiri hilo na kubadilisha hilo. Hivi ndivyo vichwa vyenu vya habari."

Baada ya matokeo mawili chanya dhidi ya Liverpool na Arsenal, Amorim alisema atajifunza zaidi kuhusu wachezaji wake wakati wa mechi dhidi ya Southampton na Brighton. United walipata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Southampton, lakini wakachapwa na Brighton.

Amorim sasa amepoteza michezo saba kati ya 15 tangu kuteuliwa kwake. United ipo nafasi ya 13 kwenye msimamo, nafasi tano na pointi 10 juu ya nafasi za kushuka daraja.

"Kila mtu hapa hafanyi vizuri, bila kujali mazingira, tunafanya vibaya na tunapaswa kukubali hilo," alisema Amorim.

"Haikubaliki kupoteza mechi nyingi sana. Kwa klabu yoyote ya Ligi Kuu England.

"Kwa hiyo ni wakati mgumu sana, lakini tunapaswa kuendelea, lazima tuendelee, hakuna njia nyingine. Tunahitaji kuteseka na kuendelea."

# *Saliba azua hofu kwa Arsenal*

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amekiri kuwa "nina wasiwasi sana" na jeraha la William Saliba baada ya beki huyo wa Arsenal kukosa katika mchezo wao wa matokeo ya sare ya mabao 2-2 dhidi ya Aston Villa, Jumamosi.



Kukosa kwa Arsenal pointi mbili za Ligi Kuu England kulichangiwa na wasiwasi kuhusu Saliba, ambaye hata hakuwapo kikosini baada ya kupata jeraha la misuli ya paja katika ushindi wa 2-1 dhidi ya Tottenham Hotspur katikati ya wiki.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ufaransa ni muhimu kwa safu ya ulinzi ya Arsenal na kukosekana kwake kutokana na jeraha la mgongo katika kipindi cha pili cha msimu wa 2022-2023 kulidhoofisha nafasi yao ya mbio za ubingwa dhidi ya Manchester City.

"Nadhani kesho (leo) tutakuwa na taarifa zaidi, tutakuwa na vipimo zaidi juu yake na tutaweka wazi zaidi kila kitu juu yake," alisema Arteta.

"Kwa hakika tuna wasiwasi], hasa kwa idadi tuliyo nayo kwenye kikosi na kuangalia benchi letu. Nina wasiwasi sana."

Arteta alilazimika kubadilisha safu yake ya ulinzi huku Jurrien Timber akihamia katikati pamoja na Gabriel na kiungo Thomas Partey akicheza kama beki wa kulia wa muda. Arsenal waliongoza kwa 2-0 kwa mabao ya Gabriel Martinelli na Kai Havertz, lakini Villa walisawazisha kupitia Ollie Watkins na Youri Tielemans.

Arteta aliisifia timu yake, lakini alikosoa safu ya ulinzi kwa bao la pili huku Matty Cash akiruka juu ya mpira, lakini akapitwa na Watkins.

"Tunaweza kujilaumu pia kwa sababu kulinda jinsi tulivyofanya haswa kwa bao moja, haiwezi kuwa sehemu ya mchezo wetu ikiwa tunataka kuwa katika kiwango cha juu zaidi," alisema Arteta.

Saliba akiwapo kwenye kikosi cha Arsenal wamekuwa na kiwango cha ushindi cha asilimia 72 huku katika michezo ambayo amekosa tangu ajiunge nayo wamepata ushindi kwa asilimia hadi 38.

# Guardiola: City sasa imerejea

**MANCHEASTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema kikosi chake kimerejea katika hali yake ya zamani baada ya ushindi wa mabao 6-0 dhidi ya Ipswich Town Jumapili na kuwaingiza katika nafasi nne bora za Ligi Kuu England.

Katika mchezo huo, Phil Foden akifunga mara mbili na kutengeneza bao lingine na Erling Haaland pia akafunga bao katika ushindi uliohitajika sana na kuwapeleka hadi nafasi ya nne kwenye msimamo wakiwa na pointi 38.

"Tumefurahi sana, tumerejea kufanya mambo ambayo yameitambulisha timu hii kwa miaka 10 iliyopita. Nimefurahishwa sana na pointi tatu na kupanda katika nafasi za kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa msimu ujao," alisema Guardiola akiambia Sky Sports baada ya mechi.

Baada ya juhudi zisizoridhisha kila upande kipindi cha Krismasi, hatimaye City walipata mwanya wao dhidi ya Ipswich, huku Guardiola akifurahishwa na jinsi timu yake ilivyocheza.

"Bora zaidi, labda si bora, lakini karibu na uthabiti tulionao katika mchezo wetu kila mtu aliye na mpira alikuwa mwerevu, mwepesi na mwenye haraka. Huwezi kuwa mwepesi ikiwa haujaunganishwa kwa kujilinda," aliongeza Guardiola.

Kwa Ipswich wao wamebakia katika nafasi ya 18 kwenye msimamo wakiwa na pointi 16.



## Fadlu: Hatuiogopi...

INATOKA UKURASA 24

furahi Simba kucheza bila mashabiki, aliipongeza timu hiyo, akisema ilicheza vizuri zaidi kuliko alivyodhania.

"Mchezo ulikuwa mgumu sana, kipindi cha kwanza tulikuwa vizuri, lakini cha pili wachezaji wangu walionekana kuchoka, Simba ilionekana kutawala zaidi, hatukuweza kuhimili mashambulizi.

"Mwanzo tulidhani kukosekana kwa mashabiki ingetusaidia kucheza vizuri bila presha maana wanajulikana Afrika kwa kuwapa morali wachezaji wao ili kushinda, lakini nimeshangazwa wamecheza vizuri zaidi ya nilivyotarajia, nawapongeza kwa hilo," alisema.

Kocha huyo ambaye timu yake imeshika nafasi ya pili, ikitarajiwa kucheza hatua ya robo fainali na zilizoshika nafasi ya kwanza makundi mengine, alisema angependa kukutana na wapinzani wao kutoka nchi moja, USM Alger.

"Mimi ningependa zaidi kukutana na wapinzani wetu USM Alger kwa sababu moja kati ya timu ya Algeria, itakuwa imejikatia tiketi ya kwenda nusu fainali

"Ningependa zaidi kukutana na wapinzani wetu USM Alger kwa sababu mbalimbali ambazo sitozisema hapa, lakini moja kati ya timu ikishinda itakuwa imejikatia tiketi ya kwenda nusu fainali itakuwa ni faida kwa nchi ya Algeria," alisema kocha huyo.

Ikumbukwe pia Novemba 21, mwaka jana, CS Constantine ikiwa nyumbani iliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya USM Alger zilipokutana kwenye mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Algeria, jambo ambalo linaonesha kocha huyo anajua anaweza kuwamudu wapinzani wao hao.

## Yanga: Ahsanteni...

INATOKA UKURASA 24

sewa na nini kifanyike, akisema mawazo yote yamekusanywa na wanayafanyiwa kazi.

"Unapokuwa kiongozi unakusanya kila kitu, kwa wanaosema hatukujipanga vizuri sawa, wanaotushauri tumekusanya ushauri wao na tunaufanyia kazi, ila kwa sasa kazi tuliokuwa nayo ni kukusanya makombe yetu, la Ligi Kuu na Kombe la FA, ili msimu ujao turudi tena kwa ngumu kubwa," alisema.

Uongozi uliwashukuru wanachama na mashabiki wote walioungana mkono kwa njia moja ama nyingine kufika hapo walipofika, pamoja na wale waliokuwa wakifika uwanjani, hususan kwenye mchezo wa mwisho Jumamosi iliyopita.

"Shukrani kwa wanachama na mashabiki wote wa Yanga waliofika Uwanja wa Mkapa, Jumamosi iliyopita. Uwapo wenu na sauti zenu zilikuwa na thamani kubwa sana. Kumepambazuka, ni siku mpya, ya jana yameshapita yatupasa kusahau. Kila huzuni tuliyonayo moyoni, tuigeuze kuwa hamasa ya kutupa morali ya kuupambania ubingwa wetu wa Ligi Kuu na Kombe la FA," alisema.

# KALLY AMTABIRIA CHILUNDA KUFANYA MAKUBWA KMC FC

**Na Adam Fungamwangwo**

KOCHA Mkuu wa KMC, Kalimangonga Ongalla, amesema ana uhakika na straika wake mpya, Shaaban Chilunda, kufanya vizuri Ligi Kuu Tanzania Bara itakayoingia kwenye mzunguko wa pili, mwanzoni mwa mwezi ujao.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Kally alisema usajili wa mchezaji huyo ni pendekezo lake kwa ajili ya kuongeza nguvu kwenye eneo la ushambuliaji, hivyo ana uhakika na alichokifanya.

Alisema anamfahamu Chilunda kwa sababu alikuwa naye Azam FC, na walifanya naye kazi nzuri, ndiyo maana amemvuta KMC.

"Tumesajili wachezaji kadhaa, wote ni kwa mapendekezo ya benchi la ufundi, tumemsajili Chilunda, ni straika mzuri sana, mimi namfahamu nimefanya naye kazi nikiwa Azam FC, naamini kabisa kuwa kwa kushirikiana na wachezaji wengine ataleta mabadiliko makubwa kwenye kikosi, hasa sehemu ya ushambuliaji," alisema Kally.


Chilunda, amerejea tena KMC kwa mara ya pili, kwani aliichezea timu hiyo kwa mkopo Januari mwaka jana akitokea Simba ingawa aliachana nayo Julai mwaka jana.

**Kabla ya hapo, alikuwa mchezaji wa Azam FC, baadaye akaenda kucheza soka la kulipwa Klabu ya CD Tenerife ya Hispania na Moghreb Atletico Tetouan ya Morocco.**

Akiwa na Simba, hakufunga bao lolote kwenye Ligi Kuu Bara, na akiwa KMC alifunga moja katika mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya JKT Tanzania uliopigwa Februari 27 mwaka jana, timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1.

Kwa mujibu wa Ofisa Habari wa Klabu ya KMC, Khalid Chukuchuku, timu hiyo imesajili wachezaji watano kipindi cha dirisha dogo la usajili lililofungwa Jumatano iliyopita.

Aaliwataja baadhi yao, mbali na Chilunda kuwa ni Hamad Pipino, kutoka timu ya vijana chini ya miaka 20, Ngorongoro Heroes, na Deusdedith Okoyo akitokea Polisi Tanzania, huku wengine wawili akisema majina yao yatawekwa hadharani baada ya baadhi ya mambo kuwekwa sawa.



**KATIKATI YAO...** Kiungo mkabaji wa Brighton & Hove Albion, Carlos Baleba, akivuruga safu ya kiungo ya Manchester United kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Old Trafford juzi. Brighton ilishinda mabao 3-1. **PICHA: MTANDAO**

# *Mkwasa: Tatizo la Yanga ni 'pre season'*

**Na Mwandishi Wetu**

NAHODHA wa zamani wa Yanga na kocha wa timu hiyo, Charles Boniface Mkwasa, amesema kuondolewa kwa timu hiyo kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kushindwa kufika hatua ya robo fainali kama msimu uliopita, kumetokana na wachezaji wa timu hiyo kutokuwa na utimamu wa mwili, kitu ambacho kimechangiwa na kutokuwa na maandalizi mazuri ya mwanzo msimu huu, 'pre season.'

Mkwasa, ambaye pia ni kocha wa Timu ya Taifa chini ya miaka 20, Ngorongoro Heroes, alisema mwanzoni mwa msimu Yanga ilitumia muda mwingi kwenda kucheza mechi za kirafiki nchini Afrika Kusini kuliko kukaa kambini na kuwapa wachezaji wao mazoezi ya nguvu.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, alisema mechi ambazo Yanga ilikuwa inashinda kwa siku za karibuni ni kujituma kwa wachezaji wenyewe baada ya maneno na malalamiko kutoka kwa mashabiki, kitu ambacho pia kimesababisha kuzalisha majeruhi wengi kwa sababu hawako fiti, wanajilazimisha tu.

"Tangu msimu ulivyoanza, Yanga haikuonekana kuwa kwenye kiwango bora ambacho ilikuwa nacho misimu miwili iliyopita, na nadhani haikufanya maandalizi ya msimu 'pre season' ya kutosha, walianza tu mazoezi, wakaenda kucheza mechi za kirafiki nchini Afrika Kusini wakashinda-shinda, lakini haikuwa na msingi wa maandalizi ya mwanzo wa msimu, ndiyo maana ilipoanza ligi ikawa inashinda bao moja moja tu, mashabiki wanalalamika maana walizoea mabao mengi," alisema.

Alisema kipindi kile kilikuwa ni cha kuwaweka wachezaji kambini na kuwafanyisha mazoezi ya kusaka fiziki badala ya mechi za kirafiki ambazo wachezaji walikuwa wanafurahia zaidi kuliko kufanya mazoezi.

"Mimi navyojua mwanzo wa maandalizi, kiasi cha wiki tatu kocha anaangalia masuala ya utimamu wa mwili tu kwanza, baadaye ndiyo yanakuja mambo ya ufundi, na timu ikikamilika kwa fiziki huwezi kukuta kuna majeruhi wengi kwenye kikosi.

"Kuna kipindi utimamu unapanda na kushuka, na wanajilazimisha kwa sababu ya presha ya mashabiki, wachezaji wanapambana, wakifanya hivyo kwa sababu wanatumia nguvu kubwa, kuna wakati wanakuja vizuri, lakini walikuwa hawawezi kucheza mechi tatu kwa kasi ile ile.

"Utakuta wanazalisha majeruhi wengi kwenye kikosi na wachezaji muhimu wanakosekana inakuwa hasara kwa timu, lakini wangekuwa na msingi wa fiziki tangu awali, wasingefika hapa," alisema.

Akiizungumzia mechi ya Jumamosi, alisema wachezaji wa Yanga walikuwa wanajazana kati ambako wenzao walikuwa wamejaa, badala ya kusambaa kila eneo, ikiwamo pembeni mwa uwanja.

"MC Alger alikuwa na plani ya kuzuia, walitaka pointi moja, walikuwa na wachezaji wengi katikati, na wengine si kiungo ni mabeki waliwaweka pale kati, tatizo ni kwamba Yanga hawakutaka kubadilika walikuwa wanataka kulazimisha kupita katikati, wangejaribu kupita pembeni na kupiga zaidi krosi, kwa sababu wako wengi wangeweza hata kufanya makosa ya kushika, au kujifunga wenyewe, mchezaji pekee ambaye nilimuona akiwa kidogo anajitahidi kwenda pembeni ni Prince Dube," alisema Mkwasa.

# Michezo

Jumanne Januari 21, 2025

Nipashe




## Man Utd hali yazidi kuwa mbaya

UKURASA 22

## 'WAMBA HAWA HAPA'...



Wauaji wa Simba waliopeleka kilio Algeria kwa CS Constantine, Denis Kibu (kulia), mfungaji wa bao la kwanza na mshambuliaji Lionel Ateba anayepongezwa na kiungo Jean Charles Ahoua (mabegani), kwa kutupia chuma cha pili wakati wakishinda 2-0 kwenye mechi hiyo ya Kundi A Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# Yanga: Ahsanteni, haikuwa riziki CAF

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Yanga imesema ilifanya kila kitu kuanzia kwenye uongozi, benchi la ufundi na wachezaji kuhakikisha wanafuzu hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini haikuwa riziki yao kwa msimu huu.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe, aliwataka wanachama na mashabiki wa timu hiyo kuwa watulivu na wavumilivu kwa wanachopitia hivi sasa, kwani wanajipanga kwa ajili ya msimu ujao warudi na nguvu mpya, ikiwamo kufanya maboresho ya usajili kwenye dirisha kubwa.

Jumamosi iliyopita, Yanga ilihitimisha safari yake kwenye hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika, baada ya kulazimishwa suluhu dhidi ya MC Alger ya Algeria kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, matokeo ambayo hayakutosha kuifanya ifuzu hatua ya robo fainali, badala yake kumaliza Kundi A, ikiwa nafasi ya tatu, ikimaliza nafasi ya tatu, ikizipa nafasi MC Alger na Al Hilal Omdurman ya Sudan kusonga mbele.

"Haikuwa riziki. Hicho ndicho nachoweza kusema. Tumshukuru Mungu kwa sababu watu wote waliokwenda uwanjani, walikwenda kuona Yanga ikifuzu robo fainali, kilichotokea kila mtu ameona, si riziki, tutajipanga wakati ujao, nadhani tutafanya maboresho msimu ujao, kila ambacho tunaweza kufanya kilifanyika ili tufuzu jamaa walikuwa vizuri sana," alisema Kamwe.

Alisema kwa sasa kumekuwa na maoni mengi kutoka kwa wanachama, mashabiki na wadau wa soka kuhusu nini kiliko-

INAENDELEA UKURASA 23

# FADLU: HATUIOGOPI TIMU YOYOTE SHIRIKISHO AFRIKA

**Na Adam Fungamwango**

## ●●● Asema kazi ndio imeanza hata vinara wa makundi waje, Kocha CS Constantine yeye aitaka USM Alger robo...

WAKATI Simba ikitarajiwa kukutana na timu moja kati ya Stellenbosch ya Afrika Kusini, Asec Mimosas ya Ivory Coast au Al Masry ya Misri, Kocha Mkuu wa Klabu hiyo, Fadlu Davids, amesema haiogopi timu yoyote ambayo watapangwa kucheza nayo hatua ya Robo Fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika.

**Aidha, amesema lengo la kutaka kuongoza kundi lilikuwa na nia moja tu ya kuanzia mechi ugenini na kupata faida ya kumalizia nyumbani na si vinginevyo.**

Fadlu alisema hayo juzi, baada ya timu yake kupata ushindi wa mabao 2-0 Jumapili iliyopita dhidi ya CS Constantine ya Algeria, ikiwa ni mechi ya mwisho Kundi A, Kombe la Shirikisho Afrika, iliyochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Alisema haiogopi timu yoyote hata zile ambazo zimemaliza nafasi ya kwanza angepambana nazo vizuri tu, lakini alipigania zaidi kushinda ili kuongoza kundi kwa ajili ya kumalizia mechi nyumbani bila kujali ni timu gani atakayocheza nayo.

"Tumepata tulichokitaka, nacho ni kumalizia nyumbani tu na kuanzia ugenini, wala hatujali tutacheza na nani, hata hizo timu zilizomaliza juu ya makundi tungeweza kucheza nazo, na tutacheza nazo kama tukivuka hapa.

"Kwa mimi hapa, michuano ya Kombe la Shirikisho sasa ndiyo inaanza. Tunafahamu kufika robo fainali ni mafanikio, lakini kwetu hatuwezi kushangilia sana. Ni mashabiki tu ndiyo wanaopaswa kushangilia kwa sababu ni rekodi na mafanikio ya klabu, lakini kwangu nimewaambia, wachezaji wangu nimewaambia, wasishangilie sana mashindano yenyewe ndiyo yanaanza sasa tunatakiwa kuhakikisha tunakuwa tayari kwa robo fainali," alisema Fadlu.

Kuhusu mechi hiyo, alisema awali wachezaji wake waliathirika kucheza bila mashabiki, lakini baadaye walizoea.

"Tulicheza mechi bila mashabiki, mwanzo iliathiri timu yangu kwa kiasi fulani, lakini baadaye walizoea, napenda kuwashukuru wachezaji wangu wameonekana wameanza kukomaa kiasi cha kutosha, toka siku ya kwanza tulipocheza michezo hii dhidi ya Al Ahli Tripoli ya Libya, hadi leo, kikosi kinaonekana kujengeka na kuwa imara siku hadi siku, wakiwa na mpira wanafanya kazi, na wanapokuwa hawana mpira wanasaidiana kuutafuta," alisema.

Simba itakutana na timu moja kati ya tatu zilizoshika nafasi ya pili kwenye makundi mengine, Stellenbosch, kutoka Kundi B, Asec Mimosas kutoka Kundi C ama Al Masry kutoka Kundi D.

Mechi za kwanza zitachezwa kati ya Machi 28 hadi 30, Simba na timu zingine zilizoshika nafasi ya kwanza kwenye makundi yao ambazo ni RSB Berkane ya Morocco kutoka Kundi B, USM Alger ya Algeria kutoka Kundi C pamoja na Zamalek ya Misri kutoka Kundi D, zikianzia ugenini na mechi za marudiano zitachezwa, Aprili 4 hadi 6 nyumbani, ambapo Wekundu wa Msimbazi watamalizia mechi yake Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Kocha Mkuu wa CS Constantine, Kheireddine Madoui, ambaye awali alionekana ku-

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >